# Nipashe

Ijumaa Novemba 17, 2023 • Tanzania 1000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581497

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**MWINYI** atumbua ma-DC wawili, ateua ma-RC

UKURASA 3



**MVUA** yabomoa nyumba 29, mtu mmoja afariki

UKURASA 4

**AFRIKA** Kusini yaishtaki Israel ICC

UKURASA 19



**MOURINHO AIPA NAFASI INTER MILAN**

UKURASA 22

# Mjadala mzito sheria uchaguzi

UKURASA 2



**"Kuwapo na mchakato wa uwazi wa kusaili wajumbe wa Tume ili wananchi wawapime kwa sifa zao." Hamad Rashid Mohammed**



**"Nimeshuhudia kuna wagombea wakinunua wengine ili wapite bila kupingwa. Marekebisho haya yatasaidia wagombea wachaguliwe kihalali." Joseph Selasini.**



**"Sheria ya Jeshi la Polisi kuhusu mikutano ifanyiwe marekebisho ili wanachama na wanasiasa wapate uhuru bila kudhibitiwa." – Juma Duni Haji.**



**"Ushirikishwaji wa wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum katika uchaguzi utaongezeka kama kutakuwapo na sheria na sera zinazowabeba." Dr. Rose Reuben.**



**"Kifungu cha sheria ambacho kinataka baada ya kupiga kura masanduku yabebwe kupelekwa eneo lingine kirekebishwe. Badala yake kura zihesabiwe na kubandikwa katika eneo ambalo uchaguzi umefanyika." Deodatis Balile.**



**"Ni vyema wadau watoe maoni ndani ya vyama vyao ili mifumo ibadilike kwa sura ambayo wanawake watapewa nafasi kubwa." Dk. Tulia Ackson.**

# Papa Francis apiga marufuku waumini kujiunga Freemasons

UKURASA 19



## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**WAFUGAJI WADAIWA KUJERUHI ASKARI**

ASKARI wa Wanyamapori wa Vijiji (VGS) pamoja...

UKURASA WA 22

**NEVILLE ANA WASIWASI ARSENAL KUTWAA UBINGWA**

GWIJI wa Soka Gary Neville anaamini kwamba, Arsenal wanaweza kushinda Ligi Kuu ya England...

UKURASA WA 24

**YANGA KUIBOMOA TENA AS VITA**

WAKATI dirisha dogo la usajili likikaribia, Klabu ya Yanga inadaiwa kupiga tena hodi Jamhuri ya Kidemokrasia...

**Mwalimu aangua kilio kisa mume kufukuzwa kazi**

UKURASA 3

**MICHEZO** VIONGOZI SIMBA WAWAWEKA KITIMOTO WACHEZAJI UK. 24

**KATUNI** UK. 6

HABARI KITAIFA



Washtakiwa wa kesi ya kumteka Hani Nooh mkazi wa Masaki Dar es Salaam na kushinikiza walipwe kiasi cha zaidi ya Sh. bilioni 8, wakielekea Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam jana kusikiliza mashtaka yanayowakabili. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Mjadala mzito sheria uchaguzi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MJADALA mzito ulitawala jana wakati wadau wakitoa maoni kuhusu Muswada wa Sheria ya Uchaguzi, Vyama vya Siasa na Tume ya Taifa Uchaguzi huku baadhi wakishauri masuala mbalimbali yaongezwe ikiwamo uwazi kwenye mchakato wa kuwapata wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Wadau pia walishauri Sheria ya Jeshi la Polisi ifanyiwe marekebisho huku wakimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa utashi wake wa kutaka kuimarisha demokrasia.

Akizungumza kwenye mjadala wa kitaifa kuhusu miswada hiyo iliyosomwa kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa 13 wa Bunge, Mwenyekiti wa Chama cha ADC, Hamad Rashid Mohammed, alishauri kuwapo mchakato wa uwazi wa kusaili wajumbe wa NEC ili wananchi wawapime kwa sifa zao.

Pia alisema suala la uchaguzi wa Rais kwenda kupingwa mahakamani halina budi kwenda kwa hatua hasa baada ya muswada kupendekeza mgombea asiruhusiwe kupita bila kupingwa. Hamad alishauri kiwekwe kiwango cha asilimia ya kura ili kuhalalisha kuwa mteuliwa halali.

Kuhusu Katiba Mpya, alishauri kuwe na subira kwa kuwa kuna mambo ambayo yamependekezwa na kikosi kazi namna ya kufikia kuwa na Katiba mpya ikiwamo Sheria ya Tume ya Uchaguzi.

"Kwa sasa tume inasimama peke yake na sheria yake. Ni jambo zuri ambalo tunaweza kufanya marekebisho pale panapohitajika," alisema.

Kuhusu wajumbe wa tume, alipongeza utaratibu unaopendekezwa wa kufanyiwa usaili lakini akashauri makundi ya wenye uulemavu na wazee yapewe kipaumbele. Alishauri tume isimamie uchaguzi mkuu na wa serikali za mitaa kama ilivyopendekezwa na kikosi kazi.

"Rais wetu ametuonesha utashi wa kisiasa. Ni kweli anataka mabadiliko ya dhati na si rahisi kwa Rais aliyeko madarakani kupendekeza utaratibu ambao unaweza kumwondoa. Huyu ni mtu mwadilifu na huu ni mchango wake mkubwa kwenye kukuza demokrasia na mabadiliko haya yatasaidia nchi. Si lazima twende na yote kwa mara moja tufanye polepole "alisema.

KULIKUWA GIZA

Makamu Mwenyekiti wa NCCR - Mageuzi, Joseph Selasini, alisema kwa miaka 60 ya uhuru wa Tanzania suala la kupita bila kupingwa limekuwa giza katika demokrasia na limesababisha matatizo mengi kwenye mfumo wa vyama vingi.

"Nimeshuhudia kuna baadhi ya wagombea wakinunua wengine ili wapite bila kupingwa. Haya marekebisho yatasaidia wagombea wachaguliwe kihalali na itasaidia wagombea kuwa huru," alisema.

Kuhusu uchaguzi wa serikali za mitaa kujumuishwa na uchaguzi mkuu, alisema itasaidia kuondokana na kupangwa kwa matokeo. Pia alishauri sheria itamke kabisa ni tume huru ya uchaguzi ili kuwalinda kisheria.

MATUMAINI MAPYA

Mwenyekiti wa ACT - Wazalendo, Juma Duni Haji, alisema kuna matumaini kupata mambo mazuri kupitia miswada hiyo na kupongeza Rais kwa utashi wa kisiasa.

"Chama cha siasa kuchagua mgombea wake wa urais ilikuwa lazima mkutano mkuu wa chama ambao ni gharama kubwa. Sheria ya Vyama vya siasa hii imeleta afueni kwamba kutakuwa na kukasimu madaraka," alisema.

Duni alishauri Sheria ya Jeshi la Polisi kuhusu mikutano ifanyiwe marekebisho ili wanachama na wanasiasa wapate uhuru bila kudhibitiwa. Pia alishauri iwekwe asilimia ya kura za kushinda kwenye urais.

Mbunge wa Viti maalum, Neema Lugangira, alisema katika suala la usawa wa kijinsia, badala ya kupendekeza vyama vya siasa kuzingatia hilo kwa makundi ya wanawake,vijana na watu wenye mahitaji maalum, linapaswa kuwapo kwa sera mahsusi.

Alisema eneo lingine ni vyama vya siasa kuwa na kanuni ambazo zitaeleleza vyama pale vinapofanya uteuzi wa wagombea katika uteuzi ama wa uchaguzi wa serikali za mitaa, uchaguzi mkuu wa wa ndani, usawa wa kijinsia uzingatiwe.

"Hili ni jamabo muhimu sana kwani nikirejea takwimu zetu za uwakilishi wa wanawake katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2019, kati ya wenyeviti wa vijiji 11,915 wanawake ni 246 sawa na asilimia 2.1 na kwenye mitaa, kati ya wenyeviti 4,171 wanawake ni 528 tu sawa asilimia 12.6 na wenyeviti wa vitongoji ni asilimia 6.7 tu.

"Pia katika Bunge kuna majimbo 264 ya uchaguzi, wanawake ni 26 tu sawa na asilimia 9.1 lakini kutokana na viti maalum wamepanda hadi asilimi 36," alisema huku akishauri kwenye muswada iwekwe asilimia badala ya kusema vyama vya sisa vizingatie usawa wa kijinsia kwa wanawake, vijana na makundi maalum.

SHERIA NA SERA

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Dk. Rose Reuben, alisema ushirikishwaji wa wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum katika uchaguzi utaongezeka kama kutakuwapo na sheria na sera zinazowabana.

"Tunahitaji idadi kubwa ya wanawake katika uchaguzi. Hii ni kwa sababu kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, kundi hilo ndilo lenye watu wengi. Ushiriki wao katika siasa ni jambo la muhimu, hivyo lazima ziwapo sera mbazo zitavilazimisha vyama kutoa usawa kwa makundi haya," alisema.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, alipendekeza kifungu cha sheria ambacho kinataka baada ya kupiga kura, masanduku yabebwe kupelekwa eneo lingine kirekebishwe, badala yake zihesabiwe na kubandikwa katika eneo ambalo uchaguzi umefanyika.

"Hiki kifungu naomba kifanyiwe marekebisho kwani kubebwa kwa masanduku ya uchaguzi humo njiani kumekuwa kukisababisha kuongezeka idadi ya kura halisi ambazo zimepigwa," alisema.

Spika wa Bunge, Dk.Tulia Ackson alimpongeza Rais kwa nia yake njema ya kusikiliza mawazo yanayotolewa na viongozi wenzake na wananchi na kuchukua hatua.

"Yale ambayo hayajakamilika kwenye hizi sheria, naamini maoni yatakayoendelea kutolewa na yatawezesha mabadiliko ya sheria zingine ambazo pengine hazijaletwa safari hii na pengine kutungwa kwa sheria mpya. Mengine yanaweza kusababisha hii miswada mingine kubadilishwa kwa maana ya vipengele au lugha ili mambo yaendelee kuwa mazuri zaidi,"alisema.

## Wafugaji wadaiwa kujeruhi askari wanyamapori, mtumishi wa halmashauri

**Na Gideon Mwakanosya,** NAMTUMBO

ASKARI wa Wanyamapori wa Vijiji (VGS) pamoja na Mtumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma, wamekatwa mapanga kwenye vichwa na jamii ya wafugaji wakati wakiwa kwenye doria ya kuwadhibiti jamii ya wafugaji wanaoendesha shughuli zao maeneo yasiyo rasmi.

Ofisa Wanyamapori na Maliasili wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, Prisca Msuha, akielezea tukio hilo alisema mtumishi, Issa Ndomondo, ambaye ni mhifadhi wanyamapori katika idara hiyo, akiwa na dereva pamoja na askari wa wanyamapori wa vijiji wapatao wanane walitekwa na wafugaji na kisha kuwacharangwa mapanga.

Alisema, mtumishi huyo akiwa na askari wasaidizi wa wanyamapori walitekwa eneo la Nakatete Kitongoji cha Milonji mamlaka ya mji mdogo wa Lusewa.

Akisimulia mkasa huo kutoka Hospitali ya Peramiho kwa simu, Issa Ndomondo alisema walitekwa na wafugaji hao wakiwa na mikuki na kuwataka wajisalimishe.

Ndomondo alidai ofisi ilipata taarifa kutoka katika uongozi wa jumuiya ya ya uhifadhi wa mazingira ya Kimbanda kuwa maeneo ya hifadhi yanahalibiwa na wafugaji kwa kukata miti ovyo na kuendesha shughuli za kilimo na kuchunga mifugo yao ndani ya hifadhi.

Ndomondo alisema kuwa walitoa taarifa ofisi ya mkurugenzi na kuanza safari ya kwenda kujiridhisha juu ya uharibifu huo, lakini wakiwa wanaelekea huko ghafla ndani ya msitu walikutana na kundi la vijana wa kifugaji wenye silaha za jadi na kuwataka wasimamishe gari na ndipo waliposimamisha na kutakiwa wajisalimishe kwa kushuka kwenye gari.

Alifafanua kuwa baada ya kushuka kwenye gari waliwahoji kuwa wanaelekea wapi, ndipo Ndomondo kudai kuwa Jumuiya ya Kimbanda imelalamika kuwa eneo lake limevamiwa na wafugaji hivyo nimetumwa kwenda kuangalia uharibifu huo kauli ambazo ziliibua hasira kwa vijana hao.

Kwa mujibu wa dereva, Juma Masuwa, baada ya kusimamisha gari na kujionea kundi la vijana hao walirudisha nyuma, lakini waliona wenzao wakishambuliwa na kundi hilo, kisha wakakimbia kusikojulikana.

Masuwa alisema waliwachukua wenzao walijeruhiwa na kuwawahisha katika Kituo cha Afya Kusewa.

Kaimu Mganga Mkuu Wilaya ya Namtumbo, Dk. Christopher Wabwarumi, alithibitisha kupokewa kwa majeruhi wawili wakiwa na majeraha mbalimbali kichwani na walipatiwa huduma za awali na kupewa rufani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, Chiriku Hamis Chilumba, alisema watu hao wanaendelea na matibabu.

Waliojeruhiwa ni Issa Ndomondo mhifadhi wanyamapori, na wengine ni askari wa wanyamapori wa vijiji Twaibu Banda, Kassimu Chai, Rashid Mbelembe, Amina Said, Mwajuma Kalumbi, Omary Komba, Ramadhani Musa na Hellena Mbunda, wanaoendelea na matibabu Hospitali ya Peramiho.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Marco Chilya, akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu alithibitisha kutokea kwa tukio hilo ambalo alisema lilitokea katika eneo la Nakatete Kitongoji cha Milonji Lusewa, wilayani Namtumbo, kwa watumishi hao kujeruhiwa wakiwa kazini.

Alisema polisi wanaendelea na uchunguzi ikiwamo kuwasaka watuhumiwa wote waliohusika na tukio hilo.

**HABARI KITAIFA**

## Familia yataka maelezo ndugu kudaiwa kufariki dunia mikononi mwa Uhamiaji

**Na Julieth Mkireri,** KAKONKO

FAMILIA ya kijana, Enos Elias Mkazi wa Kijiji cha Ilabiro, Kata ya Katanga Wilaya ya Kakonko mkoani Kigoma, ameiomba serikali kuingilia kati suala la utata wa kifo cha ndugu kilichotokea hivi karibuni na mwili wake kupatikana ukiwa umezikwa pori la Kichacha eneo la Chilambo.

Mazishi ya kijana huyo yamefanyika Novemba 15, baada ya ndugu kuutambua mwili huo wakiwa na Jeshi la Polisi, ambalo lilitoa taarifa za kuwapo kwa kaburi jipya katika pori hilo.

Wameeleza hayo jana walipotembelewa na Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, aliyefika kutoa pole kutokana na kifo cha kijana huyo ambaye mwili wake ulipatikana wiki moja baada ya kupotea kwake.

Angela Elias ambaye ni dada wa marehemu alidai mdogo wake alipotea Oktoba 27 na siku iliyofuata alimpigia simu akimwomba amtumie namba za Kitambulisho cha Taifa (NIDA), akidai amekamatwa na Idara ya Uhamiaji.

" Tulimwambia tuko shambani mbali na nyumbani tukirejea tutamtumia, lakini alipiga tena akilalamika anateseka anaomba namba hizo zitumwe haraka kwa maana alikamatwa Ijumaa na alilala polisi tukamwambia subiri baada ya hapo simu yake ilizimwa hakupatikana tena.

" Kaka Leopard tulimwambia afuatilie alienda siku ya Jumapili ofisi za Uhamiaji wakasema hawamjui na jina halijui akaenda tena Jumatatu majibu ni hayo hayo siku ya Jumanne alipoenda tena akaambiwa aende kituo cha polisi Kakonko kuulizia," alidai Anjela.

Aliendelea kudai kuwa Leopard alipofika polisi alielezwa kwamba Uhamiaji walimkamata Enos siku ya Ijumaa akaachiwa Jumamosi, wakamkabidhi Uhamiaji asubuhi na hakuonekana tena.

"Siku ya Jumatano tulifuatilia tena Uhamiaji ambao walisema walimkamata siku ya Ijumaa na kumpeleka kituo cha polisi baadaye walimwachia tukawauliza mlimpandisha gari gani wakasema sisi hatujui maana tuliwaachia wakiwa wawili tukawauliza sasa mmemweka wapi wakasema sisi hatujui na hatujui alipo.

"Baada ya hapo tulikaa kama siku mbili akatupigia simu mkuu wa kituo akasema njooni tunawahitaji tulipoenda wakasema tusubiri majibu tutawapa tulikaa siku tatu kaka akapigiwa simu akaambiwa aende na mama mzazi, walipoenda wakaambiwa waende porini kuna kaburi jipya maeneo ya kichaka na walipofukua walimtambua ndugu yao," alidai dada wa marehemu.

Baba mdogo wa kijana huyo, William Sabakwishi, alidai kupokea taarifa kutoka kwa dada yake kuhusu kifo cha utata cha Enos na alishiriki kuuzika wakiwa na ndugu wengine.

Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Kabwe alisema kutokana na taarifa hizo tayari ameshawasiliana na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na wataendelea kufuatilia wahusika wapatikane na sheria ichukue mkondo wake.

Zitto aliwaomba wanafamilia kuwa na subira wakati suala hilo wanalifuatilia, huku akisema hata kama marehemu alikuwa na utata wa uraia hakukuwa na sababu ya kutokea kifo chake kwa kuwa kila mtu ana haki ya kuishi. Siku mbili baada ya mazishi ya Enos, ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, iliunda kamati ya watu sita kuchunguza kifo cha kijana huyo aliyekuwa mkazi wa Katoro, Mkoa wa Geita.

Kwa mujibu wa Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Kigoma ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, kamati hiyo itafanya kazi kwa siku saba na kuwasilisha matokeo ili serikali ichukue hatua. Novemba 14, Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, David Misime alitoa taarifa ya kuokotwa kwa mwili wa Enos katika kijiji cha Chilambo na taarifa hiyo ilieleza kwamba kwa kushirikiana na Haki Jinai wanaendelea na uchunguzi wa tukio hilo.

Kutoka kwa wanafamilia na wananchi wa Kijiji cha Ilabiro wameomba serikali kupata maelezo ya kina kuhusu kifo cha Enos.



Ofisa Mkuu wa Uendeshaji wa Benki ya CRDB, Bruce Mwile, akizungumza katika kikao maalum cha kujadili namna sekta binafsi na mashirika yanavyotoa mchango wao kwa Sekta ya Afya nchini, kilichoongozwa na Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete (watatu kushoto), chini ya Taasisi yake ya Jakaya Mrisho Kikwete Foundation ikiwa ni sehemu ya Mkutano wa Pili wa Kisayansi wa Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto katika ukumbi wa Ruaha, Dar es Salaam. Wengine pichani ni Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI, Dk. Grace Maghembe (kulia) na David Siso, Meneja wa Programu Kanda ya Afrika Mashariki Agakhan Foundation (wa pili kushoto). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mwalimu aangua kilio kisa mumewe kufukuzwa kazi

**Na Steven William,** MUHEZA

MWALIMU wa Shule ya Sekondari Mkurumuzi, Muheza mkoani Tanga, Consolata Shayo, ameangua kilio mbele ya Katibu Tawala Mkoa wa Tanga (RAS) baada ya mume wake, ambaye ni mwalimu kufukuzwa kazi.

Mwalimu huyo na mume wa Shayo, Xavier Mrope, anadaiwa kufukuzwa kazi baada ya kwenda kumuuguza mkewe alipopata ajali wakati akitekeleza majukumu yake kazini.

Shayo aliangua kilio hicho kwenye kikao kilichoitishwa na Katibu Tawala Mkoa wa Tanga, Pili Mnyema, kwa ajili ya kusikiliza kero za watumishi wa Wilaya ya Muheza baada ya kukagua miradi ya maendeleo. Alisema mwalimu huyo alifukuzwa tangu mwaka 2018.

Shayo alisema sababu za mume wake kufukuzwa kazi ni kwamba siku moja alitumwa safari ya kikazi nje ya wilaya lakini kwa bahati mbaya alipata ajali ya gari na kuvunjika mguu na Mkuu wa Shule ya Sekondari Songa alipewa taarifa hizo.

Alisema baada ya tukio hilo, alipelekwa kupata matibabu katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) na baadaye katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, Moshi na mume wake aliomba ruhusa ili kwenda kumuuguza.

Shayo alisema akiwa bado hajapona siku ambazo mume wake alikuwa ameomba ruhusu kwa mwajiri wake ziliisha, hivyo akazidisha siku tatu zaidi na aliporejea alipewa barua ya kufukuzwa kazi.

Alisema baada ya tukio hilo, mume wake alianza kuandika barua za kujitetea kuanzia wilayani mpaka taifa pamoja na kukata rufani lakini imeshindikana na hadi sasa yuko nyumbani hana kazi yoyote.

Shayo aliongeza kuwa kutokana na mume wake kufukuzwa kazi anapata wakati mgumu kimaisha kwa kulea familia pamoja na mumewe na wazazi wa mume wake ambao ni wagonjwa.

Baada ya kutoa taarifa hiyo, alianza kuangusha kilio mbele ya RAS na viongozi wengine wa wilaya akiomba mume wake arudishwe kazini, huku watumishi wenzake wakimtuliza.

Hatua hiyo ilisababisha kikao kusimama kwa dakika kadhaa.

Baada ya kupokea malalamiko hayo, Mnyema alimwahidi mwalimu huyo kwamba ofisi yake italifanyia kazi suala hilo.

Aidha, Ofisa Mifugo Kata ya Magila, Foster Msangi, alisema tangu ameanza kazi hajawahi kulipwa fedha ya likizo zaidi ya miaka 20 na amekuwa akiandika barua kuomba fedha hizo bila mafanikio.

Naye Mratibu Elimu Kata ya Masuguru wilayani Muheza, Njingo Buzuka, alisema zaidi ya walimu 50 walipewa barua za uhamisho kutoka shule za mjini kwenda vijijini mwaka 2015 lakini mpaka sasa wanadai malipo yao na baadhi yao wameshastaafu na wengine wamefariki dunia.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Muheza, Dk. Jumaa Mhina, akijibu kero hizo, alisema ni kweli baadhi ya watumishi wanadai maslahi yao na kuwataka wale wote wanaodai fedha za likizo, uhamisho na mambo mengine, waandike barua zao na kuahidi kwamba watalipwa haki zao kwa kuwa serikali haidhulumu haki ya mtu.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Muheza, Mohamed Mfaki, alisema ofisi yake kwa kushirikiana na halmashauri, wamejipanga kushughulikia kero zote za watumishi na kuzipatia ufumbuzi.

Akifunga kikao hicho, Mnyema alisema watumishi wa Wilaya ya Muheza wanafanya kazi nzuri kwa kujituma na kwamba kero zote kuhusu maslahi yao amezisikia atazifanyia kazi.

Hata hivyo, alisema anachotaka ni kuwa mstari wa mbele kusimamia miradi ya maendeleo kuwa na ubora na kukamilika kwa wakati huku akiwapa kazi zaidi maofisa watendaji wa kata kusimamia hilo.

Pia alisema Wilaya ya Muheza inaongoza kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia na watoto huku akiwaagiza wakuu wa shule kusimamia hilo.

Mnyema alisema katika Wilaya za Muheza, Korogwe, Handeni na Lushoto kumekuwa na wimbo la watoto chini ya miaka 17 kufanya kazi za kuuza mayai, karanga na mashambani ambao wamekimbia shule huku akibainisha kuwa katika mkoa wa Tanga, watoto 8000 wamekimbia shule na jitihada zinafanyika kuwarudisha.

## Mwinyi atumbua ma-DC wawili, ateua ma-RC

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amefanya uteuzi wa wakuu wa mikoa na wilaya na kuwatumbua wakuu wa wilaya wawili.

Taarifa iliyosainiwa na Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi, Zena Ahmed Said, imesema kuwa aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Kusini Unguja, Rajab Mkasaba, ametenguliwa na nafasi yake inachukuliwa na Galos Nyimbo, ambaye ni mwanajeshi mstaafu.

Pia Mkuu wa Wilaya ya Kati Unguja, Marina Thomas, ametenguliwa na nafasi yake imechukuliwa na Sadifa Juma, ambaye alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini A, Unguja.

Kadhalika, Dk. Mwinyi amemteua, Ayoub Muhamed Mahmoud, kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, kabla ya uteuzi huo alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Ayoub ni miongoni mwa wakuu wa mikoa aliyoiongoza mikoa yote mitatu ya Unguja na ni mara ya pili kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja. Katika uteuzi huo pia Dk. Mwinyi amemteua Othman Ali Maulid, kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini A Unguja ambaye ni mstaafu wa umma.

Aidha, amemteua Rashid Hadid Rashid kuwa Mkuu wa Mkoa Kaskazini Unguja, kabla ya uteuzi huo alikuwa Mkuu wa Mkoa Kusini Unguja.

Uteuzi huo umeanza Novemba 16 na wateule hao wataapishwa Novemba 20, mwaka huu.



Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Kiula Kingu (aliyeinama na kipaza sauti), akitoa maelezo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kuhusu utekelezaji wa mradi wa maji Makongo hadi Bagamoyo wakati wa ziara ya kamati hiyo juzi walipotembelea miradi ya majisafi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Nyumba 39 zabomolewa na mvua, mmoja afariki dunia

**Na Waandishi Wetu**

NYUMBA 39 zimeanguka huku 11 zikiezuliwa mabati na kusababisha watu kadhaa kukosa makazi huku mtu mmoja akifariki dunia.

Athari hizo za mvua zimetokea katika wilaya za Nachingwea mkoani Lindi. Simanjiro (Manyara) na mkoani Songwe baada ya nyumba kubomolewa na zingine kusombwa na mafuriko yaliyotokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha katika mikoa mbalimbali nchini.

Mvua hiyo pia imesababisha madaraja kukatika na kukosekana kwa mawasiliano ya barabara katika wilaya za Simanjiro na Muheza, hivyo kusababisha huduma za usafiri kusimama.

Mbali na kusababisha maafa kwa watu kupoteza maisha na wengine kukosa makazi, mvua hizo pia zimesababisha baadhi ya maeneo kukosa mawasiliano, hivyo watu kukwama kusafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

Matukio hayo yaliyotokea kuanzia Novemba 13, mwaka huu, yameacha simanzi kwa wakazi wa maeneo hayo ambao wamelazimika kuomba makazi kwa majirani ili kujihifadhi na familia zao wakati wakisubiri msaada kutoka serikalini na wasamaria wema.

Akizungumzia maafa hayo jana, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, alisema mtu mmoja amefariki baada ya kutumbukia kwenye bwawa la maji.

Alisema nyumba 10 zilizoanguka ziko katika Kata ya Shambalahi, Wilaya ya Simanjiro na waliokosa makazi wamehifadhiwa na majirani katika Kata ya Endiamtu.

Pia alisema mvua hizo pia zimesababisha kukatika kwa mawasiliano ya barabara ya Mirerani na Naisinyai katika vijiji vya Naberera na Landai na Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA), wako kazini kurekebisha kasoro hizo.

Wilayani Muheza, Tanga, zaidi ya abiria 100 waliokuwa wakitoka Muheza mjini juzi na jana, wameshindwa kuendelea na safari baada ya Daraja la Mto Msangazi kujaa maji yaliyotokana na mafuriko.

Nipashe ilifika katika eneo la tukio na kukuta abiria wa pikipiki, bajaji na magari wakihangaika kutaka kuvuka upande wa pili ili kuendelea na safari lakini walishindwa kutokana na wingi wa maji.

Aidha, baadhi ya nyumba katika mitaa ya Genge na Kwamtiga, juzi na jana zilizingirwa na maji ya mvua kufuatia mafuriko katika Mto Amtico na kusababisha mawasiliano kukatika.

Kutokana na hali hiyo, Katibu Tawala Wilaya ya Muheza, Mohamed Mfaki, alitoa tahadhari kwa wananchi kuwa waangalifu kipindi hiki cha mvua kubwa ambayo imesababisha mito kujaa.

**NYUMBA ZABOMOKA**

Kutoka Nachingwea mkoani Lindi, nyumba 22 katika Kijiji cha Nang'olola, Kata ya Stesheni, zimeharibiwa kutokana na upepo mkali uliosababishwa na mvua kubwa zinazoendea kunyesha.

Mvua hiyo zilinyesha usiku wa kuamkia juzi na kusababisha wananchi kukosa makazi na chakula.

Kutokana na athari hizo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Mohamed Moyo, akiwa ameongozana na kamati ya ulinzi na usalama na viongozi wengine, alifika juzi kuwafariji waathirika wa maafa hayo.

Moyo aliwataka wananchi hao kuwa na utulivu wakati serikali ya ikifanya jitihada za kuwanusuru na janga hilo. Pia aliwataka wananchi kuchukua tahadhari katika kipindi hiki cha mvua ikiwamo kuhama kwenye maeneo ya mabondeni.

Wakizungumzia athari hizo, baadhi ya wananchi walioathirika na mvua hizo walisema wamekosa mahali pa kukaa na chakula kutokana na nyumba zao kuharibiwa na mvua kubwa zilizoambatana na upepo mkali uliotokea juzi.

Wananchi hao waliiomba serikali kuwatatulia tatizo la makazi pamoja chakula kutokana na changamoto ambazo wamekumbana nazo.

Hata hivyo, waliishukuru ofisi ya mkuu wa wilaya ikiongozwa na Moyo na kamati ya maafa kwa kuwatembelea na kuwafariji.

**DC AAGIZA**

Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Solomon Itunda, ameiagiza Kamati ya Maafa ya Kata ya Galula kufanya tathmini ya athari zilizosababishwa na mvua na upepo katika Kijiji cha Ilasilo na kukabidhi ripoti kwa Kamati ya Usalama ya Wilaya ndani ya siku tatu.

Alisema katika ukaguzi wa awali, kamati hiyo imebaini nyumba saba zimebomolewa huku 11 zikiwa zimeezuliwa paa baada ya mvua iliyoambatana na upepo mkali kunyesha Novemba 13, 2023 usiku katika kijiji hicho.

Mkuu wa Wilaya huyo aliwaagiza wananchi ambao nyumba zao zimebomoka kuwa watulivu wakati tathmini ikifanyika ili serikali ipate uhalisia wa athari hiyo na kuagiza uongozi wa kijiji kuhakikisha wananchi hao hawapati changamoto ya malazi wakati serikali inashughulikia tatizo hilo.

**Imeandikwa na Jaliwason Jasson (MANYARA), Ibrahim Yassin,(SONGWE) na Steven William (MUHEZA).**

# Watoto sita familia moja wafariki madai ya kula chakula chenye sumu

**Vitus Audax na Restuta Damian,** BIHARAMLO

WATOTO sita wa familia moja wa Kata ya Rusahunga, Biharamulo mkoani Kagera, wamefariki dunia baada ya kula ugali na mboga za majani ya maharage unaodhaniwa kuwa na sumu.

Baada ya kula chakula hicho, watoto hao walishindwa kupumua na baadaye kukutwa na mauti.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali Teule ya Wilaya ya Biharamulo, Dk. Dionisia Jasson, alithibitisha jana vifo hivyo vya watoto hao ambao watatu walifariki dunia katika Kituo cha Afya Nyakanazi huku watatu walifariki dunia katika hospitali hiyo.

Aliwataja waliofariki dunia kuwa ni Brian Ezekiel (miaka mitatu), Kahindi Samson (miaka tisa) mwanafunzi wa Darasa la Awali, Happiness Lazaro (12) mwanafunzi wa Darasa la Tatu wote katika Shule ya Msingi Muungano.

Wengine ni Melisiana Lazaro (11), Melina Lazaro (tisa) na Josephina Juma (miaka mitano) kutoka kwenye familia ya Lazaro Sanabanka (61).

Alisema uchunguzi wa awali wa vipimo vilivyofanyika hospitalini hapo ulibaini kuwa watoto hao walikuwa na tatizo la upumuaji lakini bado uchunguzi unaendelea katika ofisi ya mkemia mkuu wa serikali ili kubaini tatizo hilo lilisababishwa na nini.

"Watatu waliletwa hapa wakiwa na maumivu makali ya tumbo na kubanwa kifua na inasadikiwa kuwa wamekula sumu. Bado hatujapata uthibitisho wa kujua kuwa wamekula sumu kweli na ni sumu ya aina gani, hivyo kwa sasa zinaendelea taratibu za kiuchunguzi serikalini," alisema Dk. Jasson.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Blasius Chatanda, aliiambia Nipashe kuwa vifo hivyo vilitokea kwa nyakati tofauti baada ya wanafamilia wanane kula chakula cha usiku Novemba 13, mwaka huu, kisha asubuhi watoto waliamka hali zao zikiwa mbaya.

Alisema kwa mujibu wa maelezo ya wanafamilia hao, baba alikula chakula hicho hicho akiwa na watoto watatu na mama yao alikuwa na watoto wengine watatu ambao pia walikula chakula hicho.

"Awali watoto watatu walianza kujisikia vibaya mapema Novemba 14 wakakimbizwa Kituo cha Afya Nyakanazi. Wakati wanaendelea na matibabu walifariki dunia na wakati huo huo, wengine watatu walianza kujisikia vibaya nao walipelekwa katika Hospitali Teule ya Wilaya ya Biharamlo. Wakati wakiendelea na matibabu Novemba 15, nao walifariki dunia na kufanya idadi kufika sita," alisema Kamanda Chatanda.

Pia alisema wanafamilia wengine ambao walishiriki chakula hicho akiwamo mama aliyepika chakula wako salama na uchunguzi wa awali umebaini kuwa chakula kilikuwa na sumu na uchunguzi unaendelea kubaini ilikuwa ni sumu ya namna gani.

Alisema miili ya watoto watatu bado imehifadhiwa katika Kituo cha Afya Nyakanazi na watatu wengine katika Hospitali Teule ya Wilaya ya Biharamlo ambako walikuwa wakipatiwa matibabu.

Chatanda alisema kwa sasa wamechukua sampuli na kuzipeleka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali ambaye atatoa taarifa kamili ya chanzo cha vifo hivyo.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Fatma Mwassa, alieleza kupokea kwa masikitiko taarifa hizo na kutoa na kutoa pole kwa wanafamilia waliofikwa na msiba huo huku akiagiza uchunguzi wa kina kufanyika kubaini sababu za tatizo hilo.

"Pia kuna wataalamu wengine kutoka nje ya mkoa wa Kagera watakuja kwa ajili ya kuongeza nguvu katika kufanya uchunguzi huu lengo ni kujua chanzo cha suala hili lisije kujitokeza tena katika familia zetu," alisema.

Diwani wa Rusahunga, Amos Madebwa, alieleza kusikitishwa na vifo hivyo na kusema wanasubiri taarifa ya serikali ili ndugu waendelee na taratibu za mazishi ya wapendwa wao.



Muuguzi katika Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga, Wema Mshanga, akitoa huduma ya kupima afya juzi, kwa wananchi ambao wamejitokeza katika kampeni ya kupima magonjwa yasiyo ya kuambukiza ikiwamo kisukari na shinikizo la damu. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Makada 51 wajitokeza kuwania uenyekiti CCM

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAKADA 51 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, wamejitokeza kuchukua fomu kuomba kuteuliwa kuwania nafasi ya mwenyekiti wa chama hicho mkoa.

Uchaguzi huo unafanyika kuziba nafasi hiyo ambayo iko wazi kutokana na aliyekuwa anaishikilia, Dk. Stephene Mwakajumilo, kuteuliwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuwa Mkuu wa Wilaya ya Nanyumbu mkoani Mtwata.

Akizungumza na wandishi wa habari ofisini kwake jana, Katibu wa Siasa, Itikadi na Uenezi wa CCm Mkoa wa Mbeya, Christopher Uhagile, alisema kati ya wanachama hao, wanaume ni 43 na wanawake wanane.

Uhagile alisema kati ya wanachama hao, 48 wamerejesha fomu na watatu pekee hawakurudisha fomu kutokana na sababu ambazo hazijulikani na kwamba kati ya hao ambao hawajarejesha fomu, wawili ni wanaume na mmoja ni mwanamke.

Alisema idadi kubwa ya wanachama waliojitokeza kuwania nafasi hiyo inatokana na sababu mbalimbali ikiwamo kukua kwa demokrasia ndani ya chama hicho pamoja na kuondoa gharama za fomu.

"Kwa sasa kinachofuata ni vikao mbalimbali vya chama. Tutaanza na kikao cha sekretarieti, kamati ya maadili na usalama ya chama na tutamalizia na Kamati ya Siasa ya Mkoa kabla ya kuyapeleka majina haya taifa," alisema.

Uhagile aliwataka wanachama waliochukua fomu kuendelea kufuata taratibu za uchaguzi ikiwa ni pamoja na kuepuka kuanza kufanya kampeni mapema na kwamba atakayekiuka ataenguliwa kwenye mchakato.

Alisema chama hicho kimeweka taratibu mbalimbali za kuwabaini wanaokiuka misingi hiyo katika ngazi mbalimbali za chama hicho kuanzia ngazi za kata ambako kuna wajumbe wanaopiga kura.

Uhagile alisema watahakikisha wanaharakisha mchakato wa uchaguzi huo ili nafasi hiyo isikae muda mrefu bila kuwa na kiongozi.

# Simbachawene akunwa kasi ya ujenzi majengo Tume Utumishi, TAKUKURU

**Na Waandishi Wetu**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, ameridhishwa na hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa majengo ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Umma.

Pamoja na kuridhishwa huko, amewataka makandarasi kuendelea kufanya kazi kwa bidii na kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa mikataba.

Simbachawene amesema hayo kwa nyakati tofauti juzi wakati wa ziara yake ya kikazi ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa majengo hayo jijini Dodoma.

Aidha, Simbachawene alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha nyingi na kwa wakati kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya ofisi kwa taasisi zilizo chini ya ofisi yake.

"Majengo haya yameanza kujengwa wakati Mheshimiwa Rais anaingia madarakani na kulikuwa na mtikisiko wa uchumi na majanga mbalimbali duniani lakini hakusitisha kuleta fedha za ujenzi wa majengo haya. Kwahiyo hatuna budi kuendelea kumwombea dua na sala ili aendelee kutuongoza kwa hekima na busara," amesema.

Simbachawene pia aliipongeza TAKUKURU kwa ubunifu wa kulipa mkandarasi kwa mfumo wa 'milestone' lengo likiwa ni kuimarisha mtiririko wa fedha kwa mkandarasi kulingana na kazi inavyofanyika na kutoa fursa ya kukamilisha jengo kwa wakati.

Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Kamishna (CP) Salum Hamduni, alisema kwa kibali cha mamlaka ya bajeti, Mshitiri ameridhia malipo ya mkandarasi yafanyike kwa kutumia utaratibu huo badala ya kutumia utaratibu wa vyeti vya malipo ya mpito ili kukamilisha ujenzi ifikapo Julai, mwakani.

Kamishna Hamduni aliongeza kuwa mpango wa kutumia utaratibu wa malipo kwa milestone utaanza Desemba 4, mwaka huu, na utatoa fursa kwa mkandarasi kulipwa fedha kulingana na kazi alizopanga kuzifanya na kuzikamilisha kwa asilimia 100.

Wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Umma, Simbachawene alisema katika kipindi cha miezi 10, mkandarasi ambaye ni Kampuni ya CRJE (East Africa) amefanya kazi kubwa, kwa haraka na ufanisi.

"Ninawasisitiza Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kusimamia kwa ukamilifu ujenzi huu ili jengo likamilike kama linavyoonekana kwenye mchoro wa jengo hili" alisema.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma, Mathew Kirama, alisema ujenzi huo unajumuisha jengo la sakafu sita, nyumba ya mlinzi, chumba cha kuhifadhi mitambo ya umeme, kibanda cha kukusanya taka, uzio na utengenezaji wa mandhari ya nje ya jengo ambapo hadi sasa mkandarasi amefikia asilimia 50 ya kazi zote.

Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Umma ulianza Januari 12, mwaka huu na kwa mujibu wa mkataba, mkandarasi anatakiwa kukabidhi jengo hilo ifikapo Septemba, mwakani.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kampeni chanjo mifugo isimamiwe kwa umakini

**TANZANIA** imebarikiwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo ambayo kama itahudumiwa ipasavyo inaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la pato la taifa. Hata hivyo, sekta hiyo imekumbwa na changamoto mbalimbali ambazo zimesababisha kushindwa kutoa mchango wake ipasavyo.

Ziko sababu ambazo zimeifanya sekta hiyo kushindwa kuwa imara na kuleta mageuzi ya kiuchumi kwa maisha ya watu. Hatua hiyo imesababisha serikali kuanzisha mpango kabambe wa kuleta mageuzi yakiwamo ya kuwa na mifugo bora na kupenya katika soko la kimataifa la nyama kutoka Tanzania.

Katika kufanya hivyo, moja ya hatua ambazo serikali imeibuka nazo ni kuanzisha utaratibu wa kutoa chanjo ya lazima kwa mifugo, lengo likiwa kuzuia magonjwa kwa mifugo, binadamu pamoja na kuipa thamani nyama itakayouzwa katika masoko ya kimataifa.

Waziri mwenye dhamana ya Mifugo, Abdallah Ulega, akizungumza juzi na waandishi wa habari Ikulu, Dar es Salaam, alisema mifugo nchini imekuwa ikishambuliwa na magonjwa yanayosababisha athari mbalimbali zikiwamo vifo, magonjwa kwa binadamu pindi wanapokula nyama yenye vimelea vya wadudu na nyama kutokukidhi ubora katika masoko ya kimataifa.

Kutokana na hali hiyo, alisema serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, inatarajia kuanzisha kampeni ya kuchanja mifugo kwa lazima kwa utaratibu maalum, ambayo itazinduliwa hivi karibuni na Rais Samia Suluhu Hassan. Kupitia kampeni hiyo, utawekwa utaratibu maalum wa kuchanja na kwamba kama ni kila baada ya miezi mitatu, kila mfugaji atalazimika kuchanja mifugo yake.

Hatua hiyo, kwa mujibu wa Waziri, inatarajia kuiwezesha mifugo kuwa na afya bora, hivyo kuwezesha nyama ya Tanzania kupata nafasi katika soko la kimataifa. Sambamba na hayo, wananchi pia watakula nyama ambayo ni salama, hivyo kuepukana na maradhi yatokanayo na kula nyama isiyo salama.

Uamuzi wa serikali kuanzisha kampeni ya kuchanja mifugo kwa lazima ni hatua muhimu katika kuifanya Tanzania kunufaika na rasilimali hiyo adhimu, hivyo kuchanga pato la taifa.

Ni ukweli usiopingika kwamba Tanzania licha ya kuwa na mifugo mingi haijanufaika ipasavyo katika maendeleo ya uchumi kutokana na sababu mbalimbali. Kwa hatua inayotarajiwa kuchukuliwa, ni hakika itawezesha thamani ya mifugo na mazao yake kupanda na kuleta mageuzi makubwa hatimaye kupata nafasi katika soko la kimataifa ambalo mahitaji yake ni makubwa.

Pamoja na changamoto ya maradhi ya mifugo, tatizo lingine linaloikabili sekta hiyo ni ufugaji wa kienyeji usiozingatia utaalamu ndiyo maana mifugo mingi imekuwa ikikumbwa na magonjwa yanayochangia matatizo ya kiafya kwa watumiaji. Kwa mantiki hiyo, kampeni ya chanjo kwa kiasi kikubwa, itasaidia elimu ya ufugaji bora kwa wafugaji kuanzia kwa wadogo hadi wakubwa juu ya njia za kisasa za kuboresha mifugo.

Ni wakati mwafaka kwa wafugaji kuichangamkia fursa hiyo ya kuchanja mifugo ili kupatikana kwa tija na ufanisi katika sekta nzima na maendeleo ya uchumi kwa ujumla pamoja na kupunguza umaskini miongoni mwa Watanzania hususan jamii ya wafugaji.

Licha ya kuwapo kwa kampeni hiyo, ni vyema serikali ikatoa elimu kwa wananchi kuwa hatua hiyo inalenga kuwa na mifugo bora kwa manufaa ya wafugaji wenyewe na maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii. Elimu hiyo pia ilenge faida zitokanazo na uchanjaji mifugo badala ya kuendelea kufanya mambo kienyeji.

Kama ilivyo katika kampeni na mipango mbalimbali inayohusu huduma kwa wananchi, kuna wajanja wachache ambao wamekuwa wakitumia mianya hiyo kujinufaisha, hivyo ni vyema serikali ikachukua tahadhari na kutoa onyo kwa wale wote watakaojaribu kuficha dawa za chanjo au kuwalangua wafugaji wakati kazi hiyo ikiendelea.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# LATRA wako sahihi wanachokipigia debe, tuwaunge mkono kuifikia dhamira

**WATANZANIA** shime waamke sasa na kuacha kuweka pamba masikioni, vinginevyo wataangamia kwa kupoteza maisha na wengine kubaki na ulemavu wa viungo kama hawatazingatia haya.

Mamlaka ya Usafiri Ardhini (LATRA) nchini kila uchwao imekuwa ikijiongeza ili kuhakikisha abiria nchini wanakuwa salama wanaposafiri na vyombo vya moto, ili kudhibiti ajali za barabarani.

Imekuwa ikifanya hivyo, kwa kutoa elimu kwa madereva na kuwabaini wale wanaokiuka sheria za barabarani na kusababisha ajali, kwa makondakta kuuza tiketi za mabasi kwa abiria mkononi hatua chache vilipo vituo vya mabasi.

Pia, imekuwa ikiwatahadharisha wananchi kuwa makini na madereva wa teksi maarufu kama 'Uba' na 'Bolt', ambao wamekuwa wakiwashawishi abiria wao kufuta safari maarufu kama 'ku - cancel'.

Viongozi waandamizi wa LATRA, akiwamo Mkurugenzi Mkuu, Habibu Suluo, wamekuwa wakikaririwa na vyombo vya Habari, akisema vitendo hivyo vimekuwa vikifanywa na madereva na makondakta wasiokuwa waaminifu, kwa lengo la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kutoka kwa abiria huku

Katika jitihada hizo, LATRA hadi kufikia Septemba 30 mwaka huu, imekwisha kuwasajili madereva 17,990, kati ya hao 1,617 wamefanya mtihani wa mamlaka hiyo, magari mengi yamefungwa Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS).

VTS imekuwa mwenendo wa madereva wanapokuwa barabarani na kuwabaini wanaokiuka sheria na kanuni za usalama barabarani. LATRA hawajaishia hapo, kwani hivi karibuni wameanza kusimamia utoaji wa mafunzo mafupi kwa makondakta kupitia Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), baada ya kubaini kuna wanaokiuka taratibu na sheria za uendeshaji wa shughuli zao.

Baada ya kuhitimu mafunzo hayo, makondakta hao watasajiliwa kisheria na kuanza kufanya kazi zao kama ilivyofanya kwa madereva nchini.

Inaelezwa, makondakta watakaosajiliwa watakuwa wakikatwa kodi na kuiingizia serikali mapato kupitia halmashauri zao, baada ya kuingizwa kwenye mfumo maalumu.

Pia, inatajwa LATRA inawapa nafasi wasafirishaji pindi wanapokuwa katika hali ngumu kupeleka mapendekezo ya maombi ya kuongeza nauli

Kingine ni kwamba, LATRA inafanya hivyo kwa sababu haipendi kuona kila mwezi nauli katika vyombo vya usafirishaji inapanda, kutokana na sababu mbalimbali.

Ni wazi kuwa, hali hiyo inachangia kuleta taharuki ya kimaisha kwa jamii, inakaribisha athari za uchumi kwa nchi na mwananchi mmoja mmoja, kulingana na namna hali hiyo ngumu ya maisha inayochangiawa na kukosekana kipato.

Hivyo kwa ujumla, wananchi tunatakiwa kuunga mkono jitihada hizo la LATRA, kwa sababu inalenga kuondoa manung'uniko miongoni mwetu, kwa kutoa taarifa dhidi ya vitendo hivyo.

Mara kwa mara, tunaona abiria wamekuwa wakishuhudia madereva wakikiuka sheria kwa kuendesha magari kwa mwendokasi, bila ya kujali kwamba wanahatarisha maisha yao endapo ajali itatokea.

Wananchi hao hao ni mashuhuda wa madereva wanaobadili njia na kutoza nauli kubwa, lakini wanabaki kimya.

Nikibaki kwa abiria hao hao, wanapaswa kufahamu zaidi kwamba, kitendo cha wao kununua tiketi mikononi, badala ya kwenye ofisi za kampuni za mabasi, kunawaweka kwenye hatari ya ziada.

Maana yake ni kwamba, wanajiweka kando kutotambuliwa na mfumo unaotumika kuuza tiketi kielektroniki ambao ulianza kutumika nchini Julai Mosi, mwaka jana, kwa mabasi ya masafa marefu marefu, kwa sababu majina yao yanakuwa hayasomeki kwenye mfumo rasmi.

Hatari hiyo, ni pamoja na kukosekana kumbukumbu zao rasmi, idadi ya watu kwa mabasi wanayosafiri nao pindi yanapotokea majanga yanayosababishwa na ajali za barabarani, haiwi sahihi kwa takwimu rasmi.

Pia, kukosekana kumbukumbu hizo, kunamweka mtu aliyepata ulemavu wa viungo ama kufa kutokana na ajali kutolipwa fedha za bima ambazo basi husika limekatiwa kwenye kampuni mbalimbali nchini.

Juhudi zinazofanywa na LATRA ni za kupongezwa kwa sababu zinalenga kuwalinda abiria na mali zao badala ya kuwaneemesha madereva na makondakta wasiokuwa waaminifu.

Siyo abiria wa mabasi ya masafa marefu pekee yao, wa daladala nao wanapaswa kudai tiketi pale wanapolipa nauli zao wanaposafiri na kuondokana na utamaduni na kasumba iliyozoeleka katika jamii wa kutozingatia kudai tiketi.

# Mfanyabiashara alalamika kupokwa zabuni

**Na Mwandishi Wetu**

MFANYABIASHARA maarufu jijini Tanga, Sultan Salim, amemwomba Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuingilia kati mchakato wa upatikanaji wa mshindi wa zabuni ya uwendeshaji eneo la Jamhuri Park 'Forodhani', jijini humo.

Mfanyabiashara huyo ametoa malalamiko hayo baada ya kudai amedhulumiwa haki yake kutokana na mchakato ulivyofanywa hadi kupatikana mshindi huku akidai taratibu na kanuni zimekiukwa. Akizungumza na waandishi wa habari hii Dar es Salaam juzi, Salim alisema kinachoonekana watendaji wasio waaminifu wanataka kumnyima haki yake kwa makusudi kwa kuwa alistahili kushinda zabuni hiyo kutokana na dau kubwa alilotoa.

"Agosti Mosi, mwaka huu, niliomba tenda hiyo ya Jamhuri Park na nashukuru nilishinda kwa kuwa dau langu la Sh. milioni 2.2 na hakuna ambaye alilifikia siku hiyo ya ufunguzi wa zabuni hiyo.

"Lakini cha kushangaza Halmashauri ya Jiji la Tanga ilipofika Agosti 8, mwaka huu, ilitoa kusudio la upangaji na kumtangaza Ali Salim Mohamed kuwa mshindi kwa dau la Sh. mil. 2.3 wakati siku ya ufunguzi tenda hiyo alitoa dau la Sh. mil. 1.3," alisema.

Aidha, alisema anashangaa kuona mpinzani wake kutangazwa ameshinda tenda hiyo wakati siku ya ufunguzi alitoa dau dogo na yeye alitoa kubwa kitu ambacho kinampa maswali mengi bila majibu. Alisema baada ya sintofahamu hiyo, aliandika barua kwenda halmashauri kupinga matokeo hayo pamoja na kuweka zuio lakini majibu yakabaki vile vile.

"Halmashauri ilijibu kwa kutilia mkazo matokeo yao ya awali waliyoyatoa na hata nilipoandika barua ya pili kwao na kuambatanisha na nyaraka zote za mchakato mzima ulivyoanza hadi kuonyesha mimi ndiye nilipaswa kuwa mshindi, haikusaidia kitu kwani halmashauri ilikataa kupitia nyaraka zangu," alisema Salim.

Alisema kutokana na sintofahamu hiyo ndiyo maana ameamua kukimbilia kwa Waziri Mkuu Majaliwa akiamini atalifanyia kazi na ukweli kuwekwa wazi.

Mkurugenzi wa Jiji la Tanga, Said Majaliwa, alipotafutwa kuzungumzia suala hilo, alisema hafahamu lolote na kumtaka mlalamikaji kufika ofisini kwake.

"Ni kweli kulikuwa na mchakato huo wa zabauni, lakini hilo suala silifahamu na sijapata barua yoyote kutoka kwa huyo mlalamikaji. Namshauri afike ofisini kwangu ili tuone jinsi gani tunalifuatilia na kulifanyia kazi," alisema Majaliwa.

## TCRA yaimarisha miundombinu kuwezesha uchumi wa kidijitali

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imesema inaendelea kuimarisha miundombinu ya mawasiliano ili kuwezesha uchumi wa kidijitali.

Akiwasilisha mada katika mkutano wa mwaka wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Umma TCRA, Rolf Kibaja, alisema lengo ni kuchangia ujenzi wa uchumi wa buluu na kuhakikisha kila Mtanzania ananufaika.

Alisema TCRA inaendelea kuchukua hatua kuimarisha miundombinu ya mawasiliano, kuendeleza ujuzi wa kidijiti na kuhamasisha matumizi ya teknolojia za kidijiti katika sekta mbalimbali nchini.

Kibaja alisema TCRA imejizatiti kuhakikisha Tanzania inakuwa na miundombinu ya mawasiliano ya kisasa, ikitoa rasilimali masafa kwa intaneti ya kasi ya 4G na 5G ikiwa miongoni mwa hatua zilizochukuliwa na mamlaka hiyo kufanikisha uimarishaji wa uchumi wa kidijitali.

Kwa upande wa elimu, alisema TCRA inatekeleza programu za kuendeleza ujuzi wa kidijiti, ikiwa ni pamoja na kuandaa kitabu cha kuanzisha na kuratibu klabu za kidijiti katika shule, vyuo na vyuo vikuu.

Kibaja alieleza kuwa klabu hizo zinasaidia wanafunzi kujifunza kuhusu teknolojia za kidijiti na namna ya kuzitumia kwa faida yao, akitoa wito kwa wanafunzi kuanzia ngazi ya elimu ya awali hadi vyuo vikuu kujiunga na klabu za kidijiti.

Alibainisha kuwa TCRA inasisitiza kupitia kampeni zake za elimu kwa umma matumizi ya teknolojia za kidijiti katika sekta za kilimo, utalii na elimu, ikiamini kuwa teknolojia hizo zina uwezo wa kuleta mabadiliko chanya katika maisha ya wananchi.




Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ardhi, Prof. Evaristo Liwa (kulia) na Katibu wa Chuo cha Ufundi cha Chongqing cha China, Prof. Yi Jun, wakifunua kitambaa kama ishara ya kuzindua karakana ya Luban katika Taasisi ya Utafiti wa Ujenzi (IBR) inayoratibiwa na Chuo Kikuu cha Ardhi Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Bodi ya Mikopo kuanika majina wadaiwa sugu

**Na Joseph Mwendapole**

BODI ya Mikopo ya Elimu ya JUU (HESLB), imesema hivi karibuni itatangaza kwenye vyombo vya habari majina ya wadaiwa sugu wa mikopo ya elimu ya juu.

Pia imesema mwezi ujao itaanza kampeni iliyopewa jina la 'Operesheni Fichua' kwa ajili ya kuwatambua watu waliokopa lakini wamekacha kulipa licha ya kupata ajira kwenye taasisi na kampuni.

Meneja Urejeshaji na Urejeshwaji wa Bodi hiyo, George Mziray, alisema hayo juzi wakati wa mkutano wa saba wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), uliofanyika mkoani Lindi.

Alisema bodi imebaini kuwa watu wengi hasa walioajiriwa kwenye sekta binafsi, wamekuwa wakijificha kukwepa kulipa mikopo ya bodi hivyo watafichuliwa na kampeni inayokuja hivi karibuni.

"Ndiyo maana tumekuja na kampeni ya fichua, yaani ujifichue au ufichuliwe na bodi. Sasa sisi bodi tunaomba watu wanaodaiwa wajifichue wenyewe kabla ya kufichuliwa kwasababu ni wajibu wao kulipa walichokopa ili wengine wanufaike," alisema.

Alisema kwenye kampeni hiyo ambayo litakuwa endelevu, bodi itashirikiana na watendaji wa mitaa mbalimbali nchini na waajiri kupata majina ya watu ambao wameajiriwa lakini hawataki kulipa.

Hata hivyo, alisema makusanyo ya marejesho ya mikopo ya bodi ndani ya miaka mitatu iliyopita imefikia asilimia 95 ya malengo waliyokuwa wamejiwekea. "Tuko kwenye ulipaji wa kidijitali yaani hata uwe Kakonko au Nangurukuru shambani kwako ilimradi tu unasimu janja unaweza kulipa mkopo wako na ukishalipa ukaona maendeleo ya akaunti yako ya den," alisema

Alisema bodi imeunganisha mifumo ya bodi ya taasisi binafsi na za umma na kwamba wanufaika wa mikopo hiyo hawalazimiki tena kwenda kwenye bodi hiyo kufanya marejesho yao. "Tunakusanya mikopo kama mnufaika amemaliza chuo na amepata shughuli ya kumuingizia kipato au awe hakuendelea na masomo iwe imepita miaka miwili baada ya kumaliza chuo hapo tunaanza kumdai," alisema

Alisema kwa wale ambao wamejiajiri wenyewe sekta binafsi wanaweza kulipa kupitia simu zao za mkononi na wakaona maelezo yote kuhusu deni lao kwa simu.

Naye Meneja Uhusiano wa HESLB, Omega Ngole, alisema bodi imefanya maboresho mbalimbali ya mifumo yake na imekuwa ikitoa mikopo hiyo kwa wakati hali ambayo imeleta utulivu kwenye vyuo vikuu.

Alisema mwakani bodi hiyo itatimiza miaka 20 tangu kuanzishwa kwake na kwa miaka yote hiyo serikali imeshatoa jumla ya shilingi trilioni 7 na wanafunzi zaidi ya 700,000 wamenufaika.



Mkuu wa Wilaya ya Kahama Mboni Mhita kulia, akizungumza na wadau wa maji wa Halmashauri za Msalala, Ushetu na Manispaa ya Kahama katika kikao kilichoandaliwa na RUWASA-Kahama, kushoto kwake ni Kaimu Meneja wa RUWASA Mhandisi Paschal Mnyeti, Meneja wa RUWASA mkoa wa Shinyanga Mhandisi Julieth Payovela na Katibu Tawala wa Kahama Hamad Mbega jana. **PICHA; SHABAN NJIA.**

# Panya Road wavamia mtaa, wajeruhi saba

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WATU saba wamelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro baada ya kujeruhiwa na kundi la vijana wahalifu, maarufu kama panya road waliovamia makazi ya watu na kuiba vitu mbalimbali na fedha taslimu katika eneo la Majengo Mapya, Manispaa ya Morogoro.

Mmoja wa majeruhi aliolazwa katika wodi namba moja kwenye hospitali hiyo, Daudi Mnunku, alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 9:00 usiku.

Alisema akiwa amelala, alishtushwa na kelele za mwizi na ndipo alipotoka nje kusaidia majirani zake, alikutana uso kwa uso na kundi la watu takribani wanane wakiwa na silaha mbalimbali yakiwamo mapanga.

Mnunku alisema baada ya kukutana nao, walimvamia na kumpiga kwa mapanga kichwani na kufanya apoteze fahamu, hivyo kujikuta yuko hospitalini.

Majeruhi mwingine, Madula Mkone, alisema hajawahi kuwaona watu hao hata mara moja bali alikuwa anasikia tu kuhusu panya road waliomjeruhi waliomjeruhi kwenye goti na panga baada ya kuvunja mlango mkubwa na kuingia kwenye chumba chake.

Alisema baada ya kuvamiwa na kukatwa panga, alishindwa kutembea na wahalifu hao walichukua Sh. 60,000 alizoweka akiba huku wapangaji wenzake nao wakichukuliwa mali zao. Alisema baadaye wapangaji wenzake walimmchukua kwa usafiri kumwahisha hospitalini. Kwa mujibu wa Mkone, uvamizi huo haukufanyika mtaa mmoja kwa juzi bali ulianzia mtaa wa Azimio, baadaye Tushikamane na kumalizia Majengo Mapya.

Mkone alisema alishindwa kuwatambua wahalifu hao wakiwa wamevalia vilemba kichwani huku wakiwapiga na mwanga tochi machoni.

Kaimu Ofisa Uhusiano wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Morogoro, Scholastica Ndunga, alisema walipokea majeruhi saba, wote wanaume kuanzia saa !0:00 hadi 11:00 alfajiri ambao miili yao ilikuwa ikivuja damu.

Alisema majeruhi hao walionekana kujeruhiwa maeneo ya kichwa, mikono na miguu na hali zao zinaendelea vizuri huku wakiendelea na matibabu baada ya kulazwa katika hospitali hiyo. Alisema baadhi ambao wanaonekana kuwa na nafsiuu wataruhusiwa kurudi nyumbani wakati wowote.

Ndunga aliwataja majeruhi hao kuwa ni pamoja na Gerald Nashau, Daudi Mnunku na Mabula Mkone ambao wamelazwa kwenye hospitali hiyo.

Naye Diwani Viti Malum Kata ya Lukobe, Aisha Kitime, alisema mitaa katika kata hiyo ni mikubwa kuilinda yote kwa wakati bila kupata usaidizi. Aliomba Jeshi la Polisi kusaidia hata kutoa namba ili pindi linapotokea jambo kama hilo, watoe taarifa mapema.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Ally Machela, alisema kutokana na matukio kama hayo, manispaa kwa mwaka wa fedha 2023/24 imetenga Sh. milioni 50 kusaidia kukamilisha ujenzi wa kituo cha polisi kilichoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi ili kusaidia ulinzi wa kipolisi sambamba na ulinzi shirikishi.

Alisema pamoja na uwapo wa polisi kata katika eneo hilo, hakuna kituo rasmi kinachompa nafasi nzuri ya kukaa kufanya kazi na kuzuia uhalifu katika maeneo hayo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi (ACP)ACP Alex Mkama, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo huku akiwataka wananchi kuwa makini kujilinda dhidi ya vitendo vya uhalifu ambavyo vinaendelea hasa katika kipindi cha msimu huu wa mvua.

# Waandishi watakiwa kuwasilisha kazi Tuzo za EJAT mwaka 2023

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Kajubi Mkajanga, amewataka waandishi wa habari kuanza kuwasilisha kazi zao kwa ajili ya Tuzo za Umahiri za Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT).

Alibainisha hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi habari jijini hapa baada ya uzinduzi rasmi wa tuzo hizo kwa mwaka 2023.

Alisema waandishi wa habari walitakiwa kuanza kuwasilisha kazi zao kuanzia jana (Novemba 15) na mwisho wa kuwasilisha kazi hizo ni Januari 31, 2024.

Alisema kamati imeboresha kwa kuongeza makundi mapya mawili ikiwamo habari za mifuko ya hifadhi ya jamii na habari za malezi na makuzi ya awali ya mtoto huku makundi ya habari za gesi, mafuta na uchimbaji madini, sayansi na teknolojia na habari za sensa zikiondolewa katika kinyang'anyiro hicho.

"Waandishi wenye habari za maeneo haya ambao wanaona kazi zao ni nzuri wanahimizwa kuziwasilisha kupitia makundi mengine kama uchumi, biashara na fedha, au elimu au kundi la wazi kutegemea na watakavyoshauriana na wahariri wao," alisema Mukajanga.

Alisema kamati ya maandalizi ya EJAT ni mara yake ya 15 kuandaa ikiongozwa na MCT kuandaa mashindano hayo mfululizo bila kukosa na mara ya kwanza yalifanyika 2009 na lengo la tuzo hizo ni kuwatambua na kuwatuza waandishi wa habari waliofanya kazi zao vizuri.

Aliwataka waandishi wa habari wa magazeti, redio, runinga na vyombo vya habari vya mtandaoni (online) wajitokeze kuwasilisha kazi zao zilizochapishwa au kutangazwa mwaka huu kupitia njia ya mtandao (online form) au kwa kuwasilisha fomu inayopatikana kwenye tovuti ya baraza hilo.

Aliyataja makundi yanayoshindanishwa kuwa ni, Tuzo ya Uandishi wa Habari za Uchumi, Biashara na Fedha, Tuzo ya Uandishi wa Habari za Michezo na Utamaduni, Tuzo ya Uandishi wa Habari za Kilimo na Biashara ya Kilimo.

Mengine ni Tuzo ya Uandishi wa Habari za Elimu, Tuzo ya Uandishi wa Habari za Utalii na Uhifadhi, Tuzo ya Uandishi wa Habari za Uchunguzi na Tuzo ya Uandishi wa Habari za Data.

Pia, Tuzo ya Uandishi wa Habari za Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tuzo ya Uandishi wa Habari za Jinsia na Watoto, Tuzo ya Uandishi wa Habari za Walemavu, Tuzo ya Uandishi wa Habari za Afya, Tuzo ya Uandishi wa Habari za Ushirika na Tuzo ya Uandishi wa Habari za Kodi, Tozo na Mapato.

Tuzo ya Uandishi wa Habari za Hifadhi ya Jamii, Tuzo ya Uandishi wa Habari za Utunzaji wa Mazingira na Vyanzo vya Maji, Tuzo ya Uandishi wa Habari za Afya ya Uzazi, Tuzo ya Uandishi wa Habari za Malezi na Makuzi ya Awali ya Mtoto na Tuzo la kundi la Wazi.

Alisema mshindi wa jumla wa mwaka huu atapata udhamini wa Shilingi milioni tatu za masomo kwa ajili ya kujiendelea kitaaluma katika masuala ya uandishi kulingana na mahitaji yake.

Alisema Tamasha la EJAT limepangwa kufanyika Julai 27, 2024.





## Ujenzi nyumba 2,500 Msomera wafikia ukingoni

**Na Dege Masoli,** HANDENI

NYUMBA mpya za makazi 2,500 zinazojengwa na serikali katika Kijiji cha Msomera, Kata ya Misima, Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga, kwa ajili ya wafugaji wa Kimasai wanaohamia kwa hiari kutoka Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) zinatarajiwa kukamilika rasmi Disemba mwaka huu.

Akizungumza wakati akikagua maendeleo ya ujenzi huo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Hassan Abass, alisema mvua zinazoendelea kunyesha hazijaathiri shughuli hiyo kwa kuwa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT) linaendelea na ujenzi.

"Niendelee kuwaomba wananchi waliopo Ngorongoro, wanaotaka kuhamia kwenye Kijiji cha Msomera, endeleeni kujiandikisha kwa ajili ya kuhamia huko, baada ya kukamilika," alisema

Kwa mujibu wa Dk. Abbas, serikali itaendelea na azma yake ya kuwawezesha wananchi hao kuhama kwa hiari. Imeshatekeleza awamu ya kwanza ya ujenzi iliyohusisha nyumba 503, Kituo cha Polisi, nyumba ya malazi ya askari Polisi, ukarabati wa zahanati ya kijiji, shule ya msingi na sekondari.

Awami ya kwanza pia ilihusisha ujenzi wa miundombinu ya maji, majosho, barabara, umeme na mawasiliano ili kurahisisha upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii.

Dk. Abbas, alisema serikali ina nia thabiti ya kuwawezesha wananchi hao kuondoka kwa hiari, ili kupisha maboresho ya shughuli za uhifadhi Ngorongoro.

Akitoa taarifa za maendeleo ya mradi huo, Msimamizi Mkuu wa mradi huo kutoka SUMA JKT, Kanali Sadick Mihayo, alisema pamoja na mvua zinazoendelea kunyesha, kazi inaendelea kama kawaida.

# DC ataka nyoka wafugwe kulinda vyanzo vya maji

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arusha, Felician Mtahengerwa, amependekeza maeneo yenye vyanzo vya maji vinayovamiwa na wananchi kuanzisha shughuli za kiuchumi kama kilimo, ufugaji na ujenzi wa makazi, yafugwe nyoka aina ya koboko ili kuvilinda.

Amesema wanapofugwa nyoka aina ya koboko au nyuki watawafukuza waharibifu wote wa mazingira na vyanzo vya maji jambo litakalosaidia kuwapo na vyanzo vya maji vilivyo safi kwa afya ya wanandamu tofauti na hali ilivyo sasa.

Koboko ni aina ya nyoka hatari zaidi duniani kutokana na mkusanyiko wa sumu kali alionao. Ana sumu mbili zinazofanya kazi kwa pamoja na endapo mtu atang'atwa na koboko, basi ndani ya dakika tatu hadi 10, iwapo atakosa matibabu, hupoteza maisha.

Mtahengerwa alitoa ushauri huo jana wakati wa kikao cha wadau wa kidakio cha Mto Themi, kilichoitishwa juzi na Bodi ya Maji ya Mto Pangani ambacho pamoja na mambo mengine kilijadili uchafuzi wa vyanzo vya maji unaosababishwa na shughuli za binadamu. "Mnaonaje mkafuga koboko au nyuki, kwa kuwa hivi viumbe ni rafiki sana wa mazingira! hawa watafukuza waharibifu wote wanaotaka kuharibu vyanzo vya maji, lakini pia mkiona nyoka ni shida kuwaweka katika maeneo hayo; basi wekeni nyuki, nao ni walinzi wazuri sana wa maeneo kama hayo,"alisema Mtahengerwa.

Aidha, ameitaka bodi hiyo kuwaelimisha wananchi juu ya tofauti ya bodi hiyo na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Arusha (AUWSA) na Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA).

"Niwasihi Bodi ya Maji Bonde la Pangani kuendelea kutoa elimu juu ya majukumu mnayoyafanya, kwa kuwa wananchi hawajui tofauti kati ya majukumu yenu, majukumu ya Wizara ya Maji, AUWSA na RUWASA. Waelezeni vizuri ili watofautishe mamlaka hizi, "alisema Mtahengerwa.

Mkurugenzi wake, Segule Segule alisema bodi hiyo imepewa jukumu la kusimamia na kulinda vyanzo vya maji, kutoa elimu kwa wananchi juu ya utunzaji wa rasilimali maji, kutoa vibali vya uchimbaji visima na uhamasishaji upandaji wa miti katika vyanzo vya maji.

"Leo imekuwa ni siku muhimu kukutana na wadau hawa wa Kidakio Cha Mto Themi, tunasema kidakio kwa maana ya Catchment, ambayo huunganisha vyanzo vingi vya maji. Tunajua wadau hawa ni watumiaji wa maji haya kwa namna moja ama nyingine,"Segule.



Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, mkoani Manyara, Kheri James (kushoto), akizungumza kwenye kikao cha mahusiano mema cha wakazi wa Kata ya Daudi na viongozi wa Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara, kuhusu kulinda hifadhi na changamoto ya wanyama kuingia katika makazi juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Jaffo aagiza wafanyabiashara hewa ukaa kugawa maarifa

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jaffo amewaelekeza wawekezaji wanaofanya biashara ya uvunaji wa hewa ukaa nchini, kuacha kuficha taarifa kuhusiana na mradi huo endelevu wa kiuchumi ili kuisaidia jamii kujua manufaa yanayopatikana.

Alisema biashara hiyo licha ya kuchangia ukuaji wa uchumi, inafanyika kwenye misitu na wanachopaswa kukifanya wawekezaji kwa sasa ni kufuata kanuni na sheria zilizowekwa.

Jaffo, alitoa maelekezo hayo jana wakati anakabidhi hundi ya Sh. bilioni nne, kwa vijiji vya Wilaya za Mbulu na Kiteto, vinavyovuna hewa ukaa kupitia uhifadhi wa misitu. Wilaya hizo hupokea gawio la Sh. bilioni nne kutoka Kampuni ya Carbon Tanzania.

"Kuna fedha nyingi ambazo zinatokana na chanzo kimoja cha mapato cha uvunaji wa carbon kwenye halmashauri zinazohusika. Niwapongeze sana Carbon Tanzania, kwa kuisaidia jamii ya Wahadzabe kupata bima za afya ambazo huwawezesha kwenda kutibiwa Hospitali ya Kilutheri ya Haydom bila usumbufu.

"Wanajenga miundombinu ya huduma za kijamii ikiwemo shule, zahanati na vituo vya afya ili kuwarahisishia wananchi kupata huduma.

Suala la kukata bima za afya kwa wana-vijiji wote wanaotunza misitu inayotupatia carbon linawezekana. Na suala la kukata bima za afya kwa wanavijiji wote wanaotunza misitu inayotupatia kaboni linawezekana."alisema Jaffo.


Alielekeza kampuni zinazofanya biashara hiyo kuiga mfano huo kwa kuweka wazi kwa wananchi cheti cha kiasi cha hewa ukaa walichozalisha na mapato waliyokusanya.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, alimweleza Waziri Jaffo kuwa kupitia mradi huo wa uvunaji wa Carbon, wamejenga vituo vya afya, zahanati na kuboresha miundombinu ya barabara.

Sendiga alisema serikali ya mkoa huo, haitosita kumchukulia hatua mtu yeyote atakayekiuka sheria za kutunza mazingira, kwa kuwa mazingira ndio yanayotoa maji na kutunza vyanzo vya maji.

Akitoa mrejesho kuhusu uvunanji huo wa hewa ukaa, Mkurugenzi wa Fedha wa Kampuni ya Carbon Tanzania, Alphael Jackson, alisema miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana kwa jamii ya Wahadzabe wa Yaeda Chini na Eyasi ni msitu kuwa na thamani kubwa na kuajiriwa walinzi 115 wa kulinda misitu kwenye vijiji.

Mafanikio mengine, ni zaidi ya wananchi ya 1,000 kupata bima za afya, kujengwa kwa nyumba tatu za wauguzi, jamii ya Wahadzabe kupata chakula, kuchangia gharama za chakula shuleni na kujengwa kwa vyoo vya walimu 10.





# Uvuvi, ukaushaji dagaa kufanyika kidijitali

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WAVUVI wa Igombe kayenze ndogo wilayani Ilemela mkoani Mwanza wameanza kunufaika na mradi wa kidijitali wa matumizi ya mitambo ya ukaushaji dagaa pamoja na uvuvi wa kutumia taa za nishati jua zinazotumika kutega samaki na dagaa hali inayotarajia kudhibiti majanga ya moto wawapo ziwani.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa ukaguzi wa mradi huo Mkurugenzi Mkuu wa kiwanda cha ukaushaji na uchakataji dagaa cha Millennium Engineers, Diana Mbogo, alisema taa hizo zitawasaidia kuondokana na matumizi ya karabai pamoja na betri zenye kemikali ziwani.

Alisema kmpuni hiyo iliyopo chini ya ufadhili wa serikali kupita Wakala wa Nishati Vijijini (REA) imetoa taa zaidi ya 530 ambazo zinakodishwa kwa bei nafuu ya Sh.2500 kwa siku moja kwa wavuvi ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira na majanga ya moto ziwani.

Vilevile, alieleza kuwa licha ya taa hizo wametoa pia mitambo ya kisasa ambayo ni ya kwanza Afrika Mashariki inayosaidia kukausha dagaa Tani 1.2 kwa muda mfupi na kuzifanya kuwa na ubora unaokidhi viwango vya Kimataifa.

"Pia taa hii mvuvi anaweza kununua na kuimiliki yeye mwenyewe kwa gharama ya Sh.350,000 ambayo anailipa kidogo kidogo kwa miezi mitatu pia kwa mashine ya kukaushia itamgharimu Sh.300 mfanyabiashara kukausha dagaa kwa Kilo Moja," alisema Mbogo.

Mkurugenzi wa Teknolojia za Nishati Jadidifu na Mbadala kutoka REA, Mhandisi Advera Mwijage, alisema kuwa serikali imefadhili Mradi huo kwa Sh.milioni 560 sawa na asilimia 30 ya utekelezaji wake unaogharimu zaidi ya Sh.bilioni 1.5.

Alisema lengo ni kuhakikisha miradi ya nishati vijijini inakuwa na matumizi ya kiuchumi na kuzalisha fursa mbalimbali na kuhakikisha wananchi wanapata huduma kwa bei wanayoweza kuimudu ambapo zitanunuliwa taa 536 na mitambo mitatu ya kukaushia dagaa.

Mvuvi wa dagaa, Frenk Faustine, alisema kuwa uendeshaji wa mitumbwi yao unatumia mafuta ya petroli, matumizi ya mafuta ya taa yaliyokuwa yakitumika kwenye karabai yalikuwa yakisababisha mlipuko wa mara kwa mara hivyo taa hizo zimekuwa msaada wa kudhibiti majanga ziwani.

Mmoja wa Wakaushaji wa dagaa, Anna Said, alisema awali biashara yao ilikuwa na changamoto ya vifaa vya kukaushia hivyo kulazimika kuanika chini. Mvua zikinyesha dagaa walikuwa wanaharibika na kupata hasara.



Wafanyabiashara wa dagaa katika mwalo wa Igombe wakikausha dagaa kwenye vichanja, njia ambayo inatajwa kutokidhi vigezo vya dagaa bora kwa sababu hutumia siku nzima kukausha na kuwapa hasara wafanyabiashara hasa kipindi cha mvua. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Uchimbaji Almasi wadaiwa kuhatarisha vyanzo vya maji

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

SHUGHULI za kibinadamu ukiwemo uchimbaji wa Almasi unaofanyika kinyume cha sheria katika vyanzo vya maji vya Bwawa la Mhumbu na Songwa, wilayani Kishapu mkoani Shinyanga zimetajwa kuhatarisha vyanzo hivyo kutokana na uharibifu mkubwa unaoendelea.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mhandishi wa Mazingira kutoka Bodi ya Maji Bonde la Kati Nyacheli Mramba, alisema vyanzo hivyo vimevamiwa na kuanza kuharibiwa na shughuli za kibinadamu ambazo ni ufugaji,kilimo, uvuvi pamoja na uchimbaji wa almasi ambao umeacha mashimo makubwa kando ya vyanzo hivyo.

Alisema katika kudhibiti uharibifu huo, bodi imeweka alama za mipaka, mabango pamoja na kupanda miti ili kuzuia wananchi wasifanye shughuli za kibinadamu na kuwataka wananchi hao kuwa mabalozi pia wa kuvilinda visitoweke.

Akizungumza wakati wa uwekaji wa alama za mipaka kwenye vyanzo hivyo vya maji juzi, Mkuu wa Wilaya ya Kishapu Joseph Mkude, aliwaonya wachimbaji wa madini ya Almasi wilayani humo kuacha kufanya shughuli hizo kwenye vyanzo vya maji na kutafuta maeneo yaliyoruhusiwa kisheria. Alisema baada ya kuweka alama hizo za mipaka, hatarajii kuona mwananchi akikaidi na kuvamia kwenye vyanzo hivyo vya maji na kufanya shughuli za kibinadamu, ikiwamo kuingiza Mifugo na kufanya uchimbaji wa madini ya Almasi, ili kuvilinda visitoweke na kunufaisha vizazi vijavyo.

"Mtu akikamatwa kwenye vyanzo hivi vya maji akifanya shughuli za kibinadamu tutamshughulikia, kwa upande wa kunywesha mifugo kuna Matangi ya maji yamejengwa pembeni mwa mabwawa haya yatumieni na msiingize mifugo kwenye maji,"alisema Mkude.

Katika hatua nyingine, aliwataka wananchi wa Kishapu kuzitumia ipasavyo Mvua ambazo zinanyesha hivi sasa, kwa kupanda miti kwa wingi ili kuifanya Kishapu kuwa ya kijani, na kuondokana na hali ya jangwa na ukame.

Nao baadhi ya wananchi wa Songwa wilayani Kishapu, walisema uwekaji wa alama za mipaka katika mabwawa hayo, utasaidia kuvilinda vyanzo hivyo vya maji ambavyo vilikuwa hatarini kutoweka kutokana na shughuli za kibinadamu.

# Ujenzi daraja la JPM watumika kuzalisha wataalam wazawa

**Na Shaban Njia,** MWANZA

UTEKELEZAJI wa Mradi wa Ujenzi wa Daraja la Kigongo-Busisi maarufu kama Daraja la JPM unaendelea kutumika kama sehemu ya kupata wataalam wazawa wa ujenzi wa madaraja marefu kutokana na mafunzo mbalimbali yanayotolewa kwa wanafunzi pamoja wahandisi nchini.

Mpaka kukamilika kwa daraja hilo Tanzania inatarajiwa kuwa na wataalam wenye uwezo wa kutumia teknolojia ya ujenzi wa madaraja ya mifumo ya aina hiyo na kupunguza kutumia kampuni kutoka nje kutekeleza miradi.

Hayo yalibainishwa jana na Meneja wa Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS) Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Pachal Ambrose, na kuongeza kuwa mpaka sasa kuna makandarasi 14 ambao wanaojifunza teknolojia hiyo huku wanafunzi wa uhandisi wakipata fursa za mara kwa mara kujifunza katika mradi huo.

Mhandisi Ambrose alisema, wameweka idadi hiyo ya wahandisi kwenye ujenzi huo ili wajifunze teknolojia hiyo, kati yao watatu ni kutoka Tanroads na 11 ni wahitimu waliopo chini ya mpango unaoratibiwa na Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB).

"Licha ya hawa 14 wanaojifunza teknolojia hii huwa tunapokea wanafunzi kila mwaka. Mhandisi mshauri hadi sasa ana wataalamu 24 waliopo kwenye mradi, 21 ni Watanzania ambao wanashiriki moja kwa moja katika kila hatua za mradi huu."aliongeza Mhandisi Ambrose.

Mhandisi Msimamizi wa Mradi huo kutoka TANROADS, Abdukarim Majuto, alisema kuwa unatoa ajira 1,000 kila mwezi kutokana na kazi zinavyokuwa zinaendelea na mwezi Septemba 2023 ajira 813 zilitolewa kati ya hizo 770 sawa na asilimia 94.7 zilitolewa kwa Watanzania.

Alisema daraja hilo linatekelezwa na Mkandarasi China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC) kwa gharama ya Sh.bilioni 716.3. Lina urefu wa km 3.2 na litakapokamilika mwakani litarahisisha usafirishaji ndani ya Tanzania na nchi za maziwa makuu.



Ukurasa 14

Siku madiwani Magu walivyoichachamalia TARURA wakihoji barabara zisizo na 'TBS'



Waziri Mchengerwa aguswa teknolojia mbadala ya TARURA inayopunguza gharama ujenzi

Ukurasa 12

BUFE

IJUMAA NOVEMBA 17, 2023

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

## WIKI YA MWANAKATAVI...

# Mstaafu Mizengo alipopigwa na butwaa kinachoendelea nyumbani Awamu Sita

**Na Neema Hussein, MPANDA**

MNAMO Oktoba 31, kilele cha Wiki ya Mwanakatavi kilikuwa na mvuto, mgeni rasmi akiwa ni mzawa wa mkoa huo Waziri Mkuu Mstaafu Mizengo Pinda 'mtoto wa mkulima', hafla yenyewe ikimgusa kuzindua msimu wa kilimo kimkoa, kwa niaba ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Mizengo, mdau mkubwa wa kilimo nchini na aliyekuwa mbunge mkoani, akatamka:"Mimi nakaribia miaka miwili sijakanyaga huku. juzi nimekuja kila nikitupa jicho kushoto nikigeuka upande mwingine naona Mpanda inameremeta na imeanza kuzidi baadhi ya mikoa.

"Mmeitendea haki! Wiki hii mmekuja humu kila siku toka wiki imeanza na mnapokuja kuna kijifunza, naamini wengi mtatoa mawazo mbalimbali katika yale yaliwavutia.

"Maonyesho haya kwa upande mwingine ni chuo cha mafunzo ya aina mbalimbali, mtu ukipita hutakosa kutoka na wazo Fulani. Basi niwaombe sana kila mmoja atakapoondoka na kurudi alikotoka, siku ya leo tuikumbuke na kuiweka kichwani, ili tuendelee kujiandaa na wiki nyingine ya mwaka unaofuata.

"Nimepita kwenye banda moja nikaambiwa hili linashughulika na afya ya udongo, nikawauliza kwani udongo unaugua? Wakasema ndio udongo unaugua vilevile unapokosa virutubisho fulani, hata ukipanda kitu chochote haikupi matokeo."

Katibu Tawala Mkoa Katavi, Hassan Rugwa, anataja kaulimbiu ya mwaka huu ni "Imarisha uchumi kwa maendeleo endelevu," akifafanua ina msaada kwa rika na jinsia zote kujikwamua kimaendeleo na kiuchumi, akiorodhesha sekta kuu: kilimo, utalii, uwekezaji, biashara, mifugo na uvuvi.



Waziri Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda na Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko (kulia kwake), katika kilele cha Maonyesho ya Wiki ya Mwana – Katavi. **PICHA: NEEMA HUSSEIN.**

Anatoa takwimu, mwaka huu wamejitokeza waonyeshaji wa kiuchumi na kijamii 131, kati yao 14 wanatoka mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma,Tabora, Mbeya, Mwanza na Arusha.

Pia, kuna wanaohudhuria 17,256 waliopata fursa katika viwanja vya Azimio, hadi kufika Oktoba 30 na Katibu Tawala anaahidi ubunifu zaidi katika maonyesho yajayo, kupata washiriki zaidi.

**RC ANAFUNGUKA**

Mkuu wa Mkoa, Mwanamvua Mrindoko, anapokea kijiti cha ufafanuzi, akirejesha hoja mzizi wake ni mchango wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kuunga mkono mkoa huo, naye anatumia ngazi ya mgeni Mizengo kufikisha ujumbe:

"Tuendelee kumuunga mkono Rais wetu kwa kazi kubwa anazofanya kwa manufaa ya Watanzania katika mkoa wa Katavi, mheshimiwa mgeni rasmi, mkoa wetu umechangamka sana kwa kipindi hiki cha miaka takribani miwili na nusu.

" Nikupe taarifa mkoa umepokea fedha za maendeleo zaidi ya (shilingi) bilioni 806 .8 katika sekta mbalimbali, ikiwamo barabara, maji, umeme, elimu, afya, uwezeshaji wa wananchi pamoja na sekta zote zinazosimamiwa na serikali kuu pamoja na serikali za mitaa.

"Fedha hizo zimeleta matokeo chanya zimeibadilisha sana Katavi yetu! Naomba tupige makofi mengi sana kwa mheshimiwa Rais."

Anataja ishara za mabadiliko zinajumuisha kuongezeka udahili wa wanafunzi kuanzia madarasa ya awali hadi vyuoni, utoro shuleni umepungua kwa sababu wanafunzi wana miundombinu bora, walimu, pia wanapata chakula shuleni.

Mkuu wa Mkoa anafafanua kuwa, fedha zilizopatikana kwenye sekta ya elimu ni takribani shilingi bilioni 69.4, zilizojenga madarasa, majengo ya utawala kwa walimu, vyoo vya wanafunzi na walimu, maabara kwenye shule za sekondari, mabweni, mabwalo.

Pia, anasema kuna fedha zinazoitwa za'elimu bila ada' zimepelekwa kwenye shule za msingi na sekondari.

Kwa sasa anasema, kuna mradi unaoitwa 'boost'wa shule mpya 11; sita zimekamilika na zinatumika na tano ziko kwenye hatua kumaliziwa

Pia, anagusa sekta ya Afya, huduma zinatolewa karibu wamesogezewa wananchi, wakiwa na vitendea kazi vilivyoongezeka, vinawawezesha wananchi huduma za kibingwa na vipimo vya kisasa kwa afya umma.

"Tumekabidhiwa magari 12 yakiwamo ya kubeba wagonjwa sita, matano yatakwenda katika

Inaendelea Uk 12

UCHUMI

# Waziri Mchengerwa aguswa teknolojia mbadala ya TARURA inavyopunguza gharama za ujenzi

## •Aingia na mkakati kuwapa uwezo wajenzi wazawa

**Na Catherine Sungura, Dodoma**

INAJULIKANA, mtandao imara na madhubuti wa barabara za mijini na vijijini, una mchango mkubwa katika kukuza na kuimarisha uchumi wa mtu mmoja mmoja, familia jamii na taifa kwa ujumla.

Ndio katika hatua hiyo, ubunifu katika ujenzi wa barabara zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) umemvutia Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa.

Hivi karibuni Waziri Mchengerwa, ameitembelea TARURA kwa mara ya kwanza, tangu ateuliwe kwa nafasi aliyo nayo sasa.

Hakusita kuipongeza TARURA kwa kutumia teknolojia mbalimbali, zikiwamo za ujenzi wa barabara ya mawe 'cobble stone roads' na madaraja ya 'stone arch bridges'.

Anataja kilichomvuta, ni pale TARURA inafanya majaribio ya teknolojia nyingine katika kuboresha barabara wanazosimamia.

Matumizi ya teknolojia na malighafi za ujenzi zinazopatikana eneo la kazi, ikiwamo mawe katika ujenzi na matengenezo ya barabara, anataka kuongeza ufanisi, kuokoa muda na, inatunza mazingira kwa gharama nafuu.

"Matumizi ya teknolojia mbadala na malighafi zinazopatikana maeneo ya kazi kwa ajili ya ujenzi wa barabara na madaraka imeweza kupunguza gharama zaidi ya asilimia 50, TARURA imeweka kipaumbele cha kutumia malighafi zinazopatikana maeneo ya kazi ili kupata ufanisi wa gharama za ujenzi," anasema.

Takwimu za TARURA zinaeleza hadi kufikia mwezi Machi, 2023 imeshajenga madaraja 163 ya mawe yenye thamani ya Bilioni 8.7.

inatajwa gharama zimepungua na mikoa iliyojengwa madaraja hayo, idadi kwenye mabano ni; Kigoma(92), Singida (24), Tabora (5), Kilimanjaro (10), Mbeya (2), Arusha (6), Morogoro (2), Rukwa (3), Pwani (1), Ruvuma (3) na Iringa (15).

Hata hivyo, inaelezwa kuwa TARURA inaendelea kufanya majaribio ya teknolojia mbalimbali ili kutumia udongo uliopo eneo la kazi, badala ya kusomba kutoka maeneo ya mbali.

Katika ziara hiyo kwenye ofisi zake zilizopo Mji wa Serikali - Mtumba, Waziri Mchengerwa, anazungumza na menejimenti ya TARURA, watumishi wote wake wa makao makuu mkoa wa Dodoma, kujadili mambo muhimu, pia mipango ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya miundombinu na barabara za wilaya nchi nzima.

Anazitaja, barabara hizo ambazo TARURA inazisimamia kwa karibu, kuhakikisha zinatoa huduma inayokusudiwa kwa kipindi chote cha mwaka.

### MSINGI WA TARURA

TARURA ina jukumu la kusimamia matengenezo, ukarabati na ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 144,429.77.



Shughuli za ujenzi wa Barabara chini ya TARURA, zikiendelea. **PICHA: MAKTABA.**

Wakala huo, pia una majukumu mengine kama yalivyoainishwa kwenye hati ya uanzishwaji wake ikiwamo kupima.

Aidha, inafanya utafiti kuhusu vifaa vya ujenzi kupitia maabara kuu ya vifaa na utafiti, kudhibiti uzito wa magari barabarani na kulinda maeneo ya hifadhi za barabara.

Hapo, Waziri Mchengerwa anaipongeza TARURA kwa kazi kubwa na nzuri wanayofanya tangu kuanzishwa kwake.

Akawahimiza waendelee kuboresha utendaji wao katika kujenga barabara kwa viwango stahiki na kuzingatia thamani ya fedha, ili maendeleo ya kiuchumi na kijamii maeneo ya vijijini na mijini yaendelee kukua.

Anasema, tangu kuanzishwa wakala huo mwaka 2017 kumekuwapo ongezeko la barabara za lami kutoka kilomita 1,449.55 hadi kilomita 3,053.26 sawa na ongezeko la 110%.

Pia, anataja barabara za changarawe zimeongezeka kutoka kilomita 24,405.40 hadi kilomita 38,141.21 sawa na ongezeko lako la asilimia 56

"Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imeongeza fedha za matengenezo,ukarabati na ujenzi wa barabara na madaraja, kutoka shilingi bilioni 275.03 mwaka 2020/21 hadi kufikia shilingi bilioni 836.237 kwa mwaka wa fedha 2021/22,2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 204..." anatamka Mchengerwa.

### MAKANDARASI WA NDANI

Pia, Waziri Mchengerwa anaitaka TARURA kuipa kipaumbele jukumu la kukuza na kuwaendeleza makandarasi wazawa, ili kutoa mchango mkubwa kwa taifa.

Anahimiza kuzitambua kampuni za wakandarasi 20 kila mkoa, hivyo akatangaza rasmi mkakati wa kukuza na kuendeleza makandarasi wazawa.

Katika hilo, anaeleza kuwa hatua hiyo inalenga wafikie viwango vya kimataifa vya ubora na usalama na kuongeza kwamba serikali imejipanga vyema kuhakikisha inawanyanyua wakandarasi wazawa.

"Hatuwezi kuitenganisha TARURA na wakandarasi wa ndani kama ambavyo huwezi kuitenganisha TAMISEMI na wananchi.Maendeleo ya miundombinu yanamchango katika uchumi wa wananchi na wa Taifa," anasisitiza.

Anaongeza: "Mikakati ya TARURA ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2025 tuwe tumeboresha barabara za vijijini na mijini kwa asilimia 85.

"Tukiwa tunaenda kuyafikia mafanikio hayo, lazima tujiulize tumewakuza na kuwajenga makandarasi wangapi wazawa, tumewanyanyua kiasi gani kufikia viwango vya kuwafanya washindane kimataifa?

"Kwahiyo, ninawataka, pamoja na majukumu mengi mliyonayo TARURA, kwenye uongozi wangu kama waziri, jukumu la kukuza na kuwaendeleza makandarasi wazawa nitalipa kipaumbele cha hali ya juu.

Ni dhana ambayo Waziri Mchengerwa anaendelea nayo kuwa: " Leo natangaza rasmi mkakati wa kukuza na kandarasi wazawa utakaosimamiwa na ninyi TARURA.

"Nitawapa TARURA mnisaidie ili tunakokwenda tuwe tumewajenga wakandarasi, angalau kila mkoa kampuni za makandarasi 20, tutakua tumekuza kampuni za makandarasi takribani 520 katika mikoa yetu yote 26.

"Tukizishika mkono kampuni za wazawa wa Kitanzania 20 kila mkoa, ina maana tutafungua uchumi na kustawi kwa kila mkoa, pia itawezesha kuimalisha kazi za makandarasi hao kwa kila mkoa."

Anafafanua kuwa mpango mkakati huo ni wa kuziwezesha kampuni za wazawa za ujenzi ili ziweze kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa miradi inayotangazwa na TARURA.

"Lengo kuu la mpango huu ni kuboresha mazingira ambayo mjasiriamali wa Kitanzania, anaweza kufaulu, kukua na kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi," anasema.

### KASI ZAIDI

Mtendaji Mkuu wa TARURA, Mhandisi Victor Seff, anasema maagizo yote yaliyotolewa na Waziri wameyapokea na kuhakikisha watayafanyia kazi, akifafanua "ikiwamo kusimamia kazi zote zinazotelelezwa ili ziwe na ubora na zenye matokeo yanayotarajiwa na wananchi."

Nao mameneja wa wilaya na mikoa wa chombo hicho, wanaahidi kuendelea kutilia mkazo uhusiano mzuri kikazi, ikiwa ni njia ya kuepuka uzoroteshaji kazi na majkumu ya msingi.

"Hivyo, wale wote watakaowaoana wanaweza kuwaleta shida au kuwakwamisha basi hawatosita kuwachukulia hatua," anasema.

Kuhusu matumizi ya teknolojia mbadala, Mhandisi Seff anasema, ni mwelekeo wa TARURA wa kupunguza gharama na kutunza mazingira ya nchi, hivyo wataendelea kulifanyia kazi zaidi.

Anawasisitiza watumishi wenzake kuendelea kufanya kazi kutimiza malengo ya serikali kwa wakala huo. Pia, katika hoja ya kukuza mkandarasi wazawa, anasema watashirikiana na Bodi ya Wakandarasi, pia taasisi za kifedha.

"Watakuwa mstari wa mbele kwa kuifanyia kazi kwa kuwainisha wakandarasi wale wanawataka, ili waweze kutoka nje ya nchi kushindana na kuwa wa kimataifa," anabainisha.

# MSTAAFU MIZENGO ALIPOPIGWA NA BUTWAA KINACHOENDELEA NYUMBANI AWAMU SITA

Inatoka Uk 11

halmashauri zetu, kila halmashauri itapata gari moja na hospitali ya mkoa itapata gari moja, sita zilizobaki ni kwa ajili ya kuongeza ufanisi na usimamizi wa shughuli za afya katika halmashauri pamoja na ngazi za mkoa.

"Katika sekta ya Maji, miradi takribani 50 imetekelezwa katika kipindi hiki ambacho zaidi ya asilimia 51 zimekamilika na mingine inaendelea kutekelezwa na itakapokamilika, itaongeza upatikanaji wa maji vijijini kwa asilimia 83.3, kwa sasa tuna asilimia 70.7

"Tuna mradi mkubwa wa miji 28, ambao utakapokamilika utasaidia kutoka katika asilimia 60 ya upatikanaji wa maji mjini mpaka kufikia asilimia 100," anatamka Mrindoko, pia akiainisha sekta ya Umeme.

Hapo ana maelezo: "Katavi sasa hivi hung'ara, kwa sababu tayari katika vijiji 172 tulivyo navyo katika mkoa huu, vijiji 155 tayari umeme umefikia na tumebakisha vijiji 17 pekee ambavyo mkandarasi yuko saiti anaendelea na kazi na ifikapo Desemba...vitakuwa vimewasha umeme."

### HARAKATI KILIMO

Wakati Katavi inajukulikana kwa umahiri wa kilimo, Mkuu wa Mkoa ana ufafanuzi:"Katika kipindi hiki cha Dk. Samia Suluhu Hassan, miradi ya umwagiliaji minne imetengewa bajeti ya kuiendeleza.

Mkoa wa Katavi tumebarikiwa, tunayo mabonde takribani 16 ambayo yanafaa kwa kilimo cha umwagiliaji."

Ni katika eneo hilo, Waziri Mkuu Mstaafu, anaunga mkono akiwa na maoni:"Mpaka sasa wengi tunalima tu kwa sababu tumezaliwa tukafundishwa kulima, ila hata kama hatukwenda shule.

"Mzee wangu akilima miaka miwili atasema udongo wa shamba lile umepoteza sifa, sasa nilichokiona pale najua itakua na gharama, lakini ni vizuri tukubali gharama kwa ajili ya baadae, ili tuwe imara zaidi.

"Hawa wataalam tuwape muda wa kutosha wapite wilaya kwa wilaya, washuke kwenye kata, waende kwenye vijiji hadi kwenye vitongoji tukafanye uchunguzi wa udongo kwenye maeneo mbalimbali, ili watusaidie kujua nini kinakosekana katika udongo kwenye kata zetu.

"Sisi ni wafugaji wa nyuki, nimepita kwenye mabanda nimekuta wapo wafugaji. Hebu niwaombe TFS (Wakala wa Misitu) na TAWA, tuangalie namna ya kutumia misitu yetu kwa namna ambayo ni rafiki, lakini kwa maslahi makubwa zaidi kwa upande wa wananchi."

### MIUNDOMBINU NA UCHUMI

Ni eneo mkuu wa mkoa, anaeleza; "Mkoa wa Katavi sasa unafikika kwa urahisi sana na kumeleta matokeo Chanya inafikika kwa barabara ya Mpanda-Tabora, ambayo inatufikisha makao makuu ya nchi.

"Pia, inatufikisha miji ya kibiashara kama Dar es Salaam, Mwanza na mikoa mingine, hivyo mazao yetu tuna uwezo wa kupeleka popote kuyauza.

"Tuna barabara ya Kibaoni Stalike kuelekea mkoa wa Rukwa, mkandarasi yuko saiti na kazi inaendelea. Tuna barabara ya Mpanda Vikonge, kuunganisha na mkoa wa Kigoma na sasa mkandarasi yuko saiti, anajenga kuanzia Vikonge, Ruhafwe hadi Mishamo."

Mkuu wa Mkoa anaeleza; "Tunafikika pia kupitia ziwa Tanganyika, tuna bandari ya Karema ambayo imegharimu zaidi ya Bilioni 48."

Eneo lingine analotaja, ni kuwapo usafiri wa anga mara tatu kwa wiki, kutoka Mpanda mjini hadi Dar es Salaam na mikoa mingine, hali anayosema imewaleta wawekezaji, kwa sababu ya kufikika kirahisi.

Mrindiko anataja mapato ya serikali yameongezeka ndani ya miaka mitatu iliyopita, lengo la makusanyo jumla ya halmashauro zote, imefika asilimia 130.

"Kwa upande wa TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania) mapato yamefikia asilimia 100 na upande wa madini asilimia 85," anasema Mrindiko, huku akitaja kwenye viwanda, kwa miaka mitano sasa vimefikiwa 962 na 3000.

### MAZIGIRA, SAUTI YA PINDA

Kuhusu mazingira, Mrindiko anasema kuna misitu inayokabiliwa, huku kukiwapo uharibifu mdogo na kuna hatua zinachukuliwa sasa.

Vilevile anataja miradi mpya ya hewa ya ukaa, ndani ya miaka minne iliyopita, imeuingizia mkoa shilingi bilioni nane.

"Maonyesho haya yanaunga mkono jitihada za mheshimiwa Rais katika kukuza utalii, uzalishaji na uwekezaji. Tumepata maoni hapa..."anasema Mkuu wa Mkoa Mrindoko.

### HITIMISHO LA PINDA

"Ni kweli jitihada zipo, lakini sio kweli kwamba tumekamilisha kazi katika uhifadhi wa mazingira. Mimi nilitamani sana jambo hili la uhifadhi wa mazingira tulitengee mada maalum kabisa.

"Hifadhi, nimeangalia viboko, lakini wanapata shida kabisa wapo kwenye matope, kisa hakuna maji. Kwahiyo, maana yake lazima kuna mahali kwenye mto huu maalumu kunakitu kimefanyika..." anatamka Pinda, huku akinyooshea vidole mikasa ya uhalifu mkoani Katavi, ichukuliwe hatua.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Tukae 'mkao wa kula' na athari afya, mafuriko mvua zinazoendelea





**NA SABATO KASIKA**

MVUA kubwa inaendelea kunyesha jijini Dar es Salaam na maeneo mengine ya nchi na kusababisha maafa, huku baadhi ya watu wakipoteza mali baada ya maji kuingia ndani ya nyumba zao.

Tumeambiwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa, hali hii inaendelea hadi kesho Jumamosi.

Wengine nyumba zao zimebomoka na kuwaacha hawana makazi, hivyo kujikuta wakiwa katika sintofahamu, huku pia wakikabiliwa na tatizo la kiafya hasa kutoka na maji kujaa katika nyumba zao.

Kwa mazingira kama hayo, ni wazi afya zao ziko hatari, hasa baada ya maji kujaa katika nyumba, maana yake ni kwamba hata vyoo vimefurika maji hayo na kusambaa mitaani na kutishia afya zao.

Lakini maji yakiwa yamejaa kwenye vyoo na kufurika, wakati wa mvua kama huu, huwa ni fursa kwa baadhi ya watu ambao hutapisha vyoo vyao ili majitaka yachangamane na ya mvua.

Ninadhani wakati huu mvua zinapoendelea kunyesha, ni vyema kuchukua tahadhari ili wasipate madhara ya kiafya, vinginevyo inaweza kuwa rahisi kuvamiwa na magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu.

Yaani waliozoea kutapisha vyoo, waache mtindo huo, lakini pia wale ambao nyumba na vyoo vitajaa maji ya mvua, watoe taarifa kwa wataalam wa afya ili wasaidiwe jinsi ya kujinga na hali hiyo.

Kwa mujibu wa wataalam wa afya, mvua za aina hiyo husababisha utapiamlo, kipindupindu na magonjwa mengine ya kuhara, homa ya matumbo, homa ya ini na malaria.

Hivyo, ingekuwa ni vyema kama wakazi hasa wa Dar es Salaam, ambao wamekuwa na mtindo wa kutiririsha majitaka wakati wa mvua, waache mtindo huo, ili kulinda afya zao na wengine.

Lakini pia kuna haja ya kujiuliza kwa nini mafuriko yanatokea kila mwaka. "Kwa nini, watu hawajifunzi kutokana na uzoefu na kuchukua hatua mapema za kuepusha janga hilo?.

Kimsingi mafuriko ni moja ya majanga ya asili, lakini wakati mwingine ipo haja kuangalia ujengaji wa nyumba, kwani wapo baadhi ya watu wamejenga kwenye maeneo ambayo maji ya mvua yanapita.

Wakati huu ambao baadhi ya nyumba zimekumbwa na mafuriko, ni muhimu kuchukua tahadhari, kwa ajili ya kuokoa maisha, watu wasijenge katika mikondo ya maji na wasitiririshe majitaka.

Katika mkoa wa Dar es Salaam, baadhi ya maeneo ambayo kila mara huathiriwa na mafuriko ni Jangwani, Tandale, Msasani Bonde la Mpunga, Buguruni kwa Mnyamani na Bonde la Mto Kigogo.

Maeneo mengine ni Boko Basi Haya na mengine mengi ambayo ni vyema mtu kuuliza kwanza kabla ya kuhamia, kwani hujaa maji ya mvua na kusababisha watu kuhangaika huku na kule kuokoa maisha yao.

Kama nilivyoeleza awali, mafuriko ni moja ya majanga ya asili, lakini ujengaji wa nyumba katika njia za maji ya mvua na msongamano mkubwa wa makazi ya watu imekuwa ni vigumu kwa maji kupita kwenye njia yake na kusababisha mafuriko.

Ukweli ni kwamba kuna athari kubwa za kuzuia njia ya maji, kwani yakifurika huwa hayachagui mahali pa kupita, ndio maana nikaeleza kuwa husababisha mafuriko ambayo wakati mwingine yanaua.

Mvua zikiwa kubwa mito hutapika kwenye kingo zake na kusambaa maeneo ya karibu yake ambayo kwa kiasi kikubwa yamevamiwa na makazi ya watu hivyo ni rahisi kuingia katika makazi.

Mafuriko hayo yanapotokea, huzoa taka za aina, zikiwamo za chooni ambazo ni hatari kwa afya za watu, hivyo suala la kuchukua tahadhari kuanzia ujenzi na hata kutoririsha majitaka ni jambo muhimu.

**• Mwandishi wa safu hii, leo hajaweza kuwapo kutokana na sababu nje ya uwezo wetu. Mhariri.**

UCHUMI

# Siku madiwani Magu walivyoichachamalia TARURA wakihoji barabara zisizo na 'TBS'

## • RUWASA nayo yaleyale haikubaki salama

**Na Anthony Gervas, Magu**

Ni katika vikao vya halmashauri ukiwa mhimili wa dola, ndiko kunashuhudiwa misuguano, kutetea haki za umma kutoka kwa wawakilishi wa umma, madiwani, dhidi ya watoa huduma.

Katika kikao cha hivi karibuni wilayani Magu,kilibeba simulizi ya 'vuta nikuvute', mazito yakiwaelemea wasimamizi wa huduma na ujenzi wa barabara, pia maji.

Hao ni Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) wilayani Magu, pia Wakala wa Maji Mijini na Vijijini (RUWASA) wakilazimika kutoa majibu ya minong'ono na malalamiko rasmi na yasiyo rasmi.

Hayo ni yanayohusu barabarani na katika maisha ya wana – Magu kwa ujumla, vitendawili vikitegulliwa kugusa miradi ya kujenga barabara na madaraja.

Historia ya mikutano ya madiwani wilayani humo imekuwa ikibeba malalamiko ya ubovu wa miundombinu hiyo muda mfupi baada ya kujengwa.

Madiwani hao wanalalamika, kuwa ujenzi huo umekuwa ukifanyika chini ya kiwango kinachotakiwa, kwa idadi ya moramu, changarawe na mawe, hata ikageuka kero ya huduma hiyo katika jamii, ambazo hudumu muda mfupi hata kwa miezi sita tu, kabla ya kuharibika.

Vikao kadhaa vya Baraza la Madiwani vimekuwa vikiwaka moto kuhoji kitendawili kisichoteguka kuhusu usimamizi wake kudaiwa ni hafifu, huku wakiwakataa mameneja kadhaa wa Tarura katika wilaya hiyo, wasiendelee kufanya nao kazi, ambao mara nyingi wamekuwa wakihamishwa na serikali kwenda kwingine.

Madiwani hao wanaishinikiza serikali kuirudisha miradi ya barabara katika usimamizi wa halmashauri za wilaya, badala ya kudumu katika serikali kuu kupitia Tarura, wakidai kugubikwa na udanganyifu wa utafunaji fedha.

Wiki iliyopita madiwani hao waling'aka wakitaka miradi ya Tarura irudishwe usimamizi wake kwenye halmashauri, kutokana na madai ya kushindwa kusimamia, hali inayowasababishia hasara kupotea mabilioni ya fedha yanayotolewa na Rais, Dk.Samia Suluhu Hassan kutekeleza miradi hiyo.

**KILIO KILIVYO**

Diwani wa Kata ya Buajshi wilayani Magu, Lucas Deleli, anamsifu Rais kutoa fedha za kutosha katika halmashauri hiyo, kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya wananchi, ikiwamo katika sekta za elimu, maji, afya na barabara, lakini kunakosekana tija ya matumizi.



Sehemu ya barabara zinazohudumiwa na TARURA, wilayani Magu. Chini, mafundi wa mamlaka ya maji, RUWASA wakiwa kazini kusambaza maji wilayani humo. **PICHA: MTANDAO.**

Deleli anadai wameshagundua anaowaita 'mchwa' katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu, wakishirikiana na Tarura 'kutafuna' fedha za miradi ya umma na kusababisha kutekelezwa chini ya kiwango kinachotakiwa, huku kilio kikuu kikibaki kutopitika barabara na ubovu wa madaraja wilayani, hasa nyakati za mvua.

"Tangu Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan, aanze kumwaga mabilioni ya shilingi Magu kupitia Tarura kwa ajili ya kutekeleza miradi ya barabara, hadi sasa bado hazipitiki na madaraja yake, 'mchwa' uliopo Magu tumeshaujua tunaomba tabia hiyo ikome," anadai Deleli.

Diwani wa Kata ya Kongolo, Ng'wanabuta Enos, anadai kwamba wahandisi waliopo Tarura, wengi hawafungamani vya kutosha katika taaluma zao, kwa sababu wanayoyafanya hayaendani na taaluma walizo nazo.

"Tunaomba leo tuazimie madiwani, tukiona mahali barabara imeharibika kwa sababu imejengwa chini ya kiwango, wahandisi wakatwe mishahara yao ikajenge upya barabara hizo na madaraja," anasema Enos, katika lugha ya mafumbo.

Enos anadai katika kata yake ya Kongolo Barabara ya Kongolo-Rangi, haipitiki wakati kumejengwa ndani ya miezi sita tu iliyopita, akihisi barabara na madaraja hayo, hadi kufika miaka mitatu ijayo zitakuwa hazipitiki.

Diwani Kata ya Bukandwe, Marco Minze, ana madai kwamba tatizo kubwa linalochangia miradi hiyo kutodumu, inatokana na wahandisi wa ujenzi kupitisha mradi wakiwa mkoani jijini Mwanza, badala ya wilayani Magu kwenye uelewa mzuri.

**MWENYEKITI HALMASHAURI**

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu, Mpandalume Simon, anakiri kuwapo barabara na daraja bovu katika halmashauri hiyo, akiilaumu Tarura imeshindwa kusimamia miradi hiyo.

Simon anasema kuwa hata Wakala wa Maji Mijini na Vijijini(RUWASA) nao wameshindwa kusimamia vema miradi yao, akiomba serikali kuirudisha miradi hiyo katika halmashauri, badala ya kusimamiwa na serikali kuu.

"Miradi yote ya Tarura na Ruwasa irudishwe usimamizi halmashauri ya wilaya (Magu), kwa sababu wameshindwa kuisimamia vizuri," anasema Simon.

**MENEJA TARURA.**

Meneja wa Wakala wa barabara Mijini na Vijijini (TARURA) wilayani Magu, Mussa Mzimbiri, anaahidi kikaoni kwamba,nyakati za mvua, watajitahidi kuhakikisha barabara zote mbovu zinazolalamikiwa na madiwani, zinatengenezwa kwa kiwango kinachotakiwa.

"Mtandao wa barabara zote Wilaya ya Magu ni kilomita 1,524.15 nyakati hizi za mvua, tutajitahidi mkandarasi kufanya ujenzi, ili kupunguza ubovu wake ziweze kupitika," anaahidi Mzimbiri.

Katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/24 Tarura wilaya ya Magu, imetengwa shilingi bilioni 2.3 za kukarabati barabara na matengenezo.

Mzimbiri anataja kati ya fedha hizo, shilingi milioni 800 zinatoka Bodi ya Mfuko wa Barabara (Roadfund) na shilingi bilioni moja za maendeleo kupitia tozo na Mfuko wa Jimbo, shilingi milioni 500.

**SAUTI YA RUWASA.**

Katika Baraza hilo la Madiwani, pia yalitokea malalamiko ya madiwani kuhusu maumivu ya bei ya kununua maji bomba yakiumiza wananchi majumbani kutoka Wakala wa Maji Mijini na Vijijini (Ruwasa), kwamba zimekuwa kubwa kulinganishwa na gharama za maisha yao.

Meneja Ruwasa wilayani Magu, Daudi Amlima, anajitetea hakuna mbadala kufuata, kutokana na kupanda kwa gharama za uendeshaji wa mradi huo.

Anaorodhesha vyanzo vya gharama hizo vinajumuisha mishahara ya wafanyakazi wa vituo vya maji, ulinzi, matengenezo, umeme na mengine mengi kama usafiri.

Pia, anasema Ruwasa hivi sasa inatekeleza miradi minane ya maji bomba inayogharimu shilingi bilioni 18, utekelezaji wake ukifikia asilimia 60, kuwahudumia watumiaji rasmi 293,000 sawa na asilimia 75 ya walengwa. Mradi utakamilika mwezi Juni, mwaka ujao.

Anaorodhesha miradi hiyo ni Bugando-Chabula, Lugeye-Kahangala, Sagani- Mwamabanza, Nyang'hanga -Iseni, Misungwi-Lumeji na Mahaha wilayani humo, huku wakitarajia kufanya upanuzi wa miradi ya maji bomba Igombe na Kinango.





# HABARI DODOMA

## 46% ya nguvu kazi nchini hawatumii huduma za fedha

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

KAMISHNA wa Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha kutoka Wizara ya Fedha, Dk. Charles Mwamaja amesema asilimia 46.2 ya nguvu kazi nchini hawatumii huduma rasmi za fedha, hivyo kukosa fursa za koboresha maisha na uchumi.

Dk. Mwamaja alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu maadhimisho ya wiki ya huduma za fedha kitaifa yanayotarajiwa kufanyika kuanzia Novemba 20 hadi 26 mwaka huu jijini Arusha.

Alieleza kuwa takwimu hizo ni kwa mujibu wa utafiti wa Finscope wa mwaka 2023 nchini ambao unaonyesha asilimia 53.8 tu ya nguvukazi wanatumia huduma hizo rasmi za fedha.

Aidha, alisema serikali inakusudia kuwa ifikapo mwaka 2025 takribani asilimia 80 ya wananchi watakuwa wamepata uelewa wa masuala ya fedha kutokana na elimu wanayoendelea kuitoa kwa kushirikiana na wadau wa taasisi za kifedha.

Dk. Mwamaja aliyataja malengo ya huduma ya fedha kuwa ni kujenga uelewa wa weledi kwa umma katika matumizi sahihi ya huduma hizo za fedha zinazotolewa ili kujenga uchumi na kuondoa umaskini nchini.

Alisema malengo mengine ni kuimarisha ufanisi wa masoko ya fedha kupitia elimu, kuongeza upatikanaji wa huduma za fedha, kutoa elimu ya kumlinda mtumiaji wa huduma hizo za kifedha na kuwawezesha wananchi kusimamia vizuri rasilimali fedha .

Alisema pia kuwawezesha wajasiriamali wadogo kuongeza ujuzi na matumizi sahihi za huduma za fedha katika kukuza biashara zao, kuimarika kwa utamaduni wa kijiwekea akiba, kukopa na kulipa madeni na kuongezeka kwa mchango wa sekta ya fedha kwenye ukuaji wa uchumi.

Aliwataja walengwa wanaotakiwa kufikiwa kwenye wiki hiyo ya huduma ya fedha kuwa ni watumishi wa umma, wanafunzi, wanawake, vijana, wenye mahitaji maalumu, wajasiriamali wadogo na wa kati na kundi la bodaboda.

Kadhalika, alisema washiriki katika maadhimisho ni wizara, idara na wakala wa serikali wa Tanzania Bara na visiwani, wasimamizi wa sekta za fedha pamoja na taasisi za fedha, asasi zisizo za kiserikali

Hata hivyo, alisema maadhimisho hayo yanatarajiwa kuwa na matokeo chanya ya uelewa wa masuala ya fedha kutokana na walivyojipanga kuwafikia idadi kubwa ya watu.

"utoaji wa elimu ya huduma za fedha utakuwa ni endelevu na kwa maeneo ya vijijini kuna mapango maalumu endelevu wa utoaji elimu hasa kwenye maeneo ya minada na kwenye mikusanyiko mbalimbali,"alisema.




Makamu Mkuu wa Chuo cha Taaluma, Utafiti na Ushauri, Dk. George Adriano (wa tatu kushoto), akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) kuhusu mafanikio yaliyopatikana kwa miaka kumi kutoka Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Decohas kilipoanzishiwa mwaka 2014, kinachozalisha watumishi wa idara ya afya kilichoko Nala jijini Dodoma, (wa tatu kulia) mwanamuziki wa kizazi kipya Raymond Shaban (RayVany). **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Mamlaka za maji mikoa zaagizwa kuwasilisha taarifa sahihi

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imeziagiza mamlaka za maji za mikoa na miradi ya kitaifa kuwasilisha taarifa sahihi za utendaji ili kuchochea maendeleo ya sekta ya maji nchini.

Mkurugenzi wa EWURA, Mhandisi Exaudi Fatael aliyasema hayo juzi alipokuwa akifungua mkutano wa watendaji wa mamlaka za maji nchini.

Mhandisi Fatael alisema EWURA imebaini uwepo wa baadhi ya takwimu zisizo sahihi kutoka mamlaka za maji, hivyo imeitisha kikao hicho maalum ili kuhakiki usahihi wa taarifa hizo.

Alieleza kuwa baadhi ya takwimu zinazoboreshwa ni pamoja na takwimu za kiwango cha maji yanayozalishwa, muda wa huduma, usafi wa mazingira na ubora wa maji.

"EWURA huandaa taarifa ya tathmini ya utendaji wa mamlaka za maji nchini kila mwaka kwa mujibu wa Kifungu cha 29(2) cha Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira,"alisema.

Mhandisi Joviyus Mabula kutoka Wizara ya Maji, alizitaka mamlaka za maji kuhakikisha zinatoa takwimu sahihi kwa kuwa wizara hutumia takwimu hizo kupanga mipango ya sekta maji.

## DC ataka kasi usajili wakulima kupata mbolea za ruzuku

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Wilaya ya Singida, Mhandisi Paskas Muragili, amewagiza maofisa ugani kuongeza kasi ya kusajili wakulima katika daftari, ili kuwawezesha kupata mbolea na mbegu za ruzuku kwa msimu wa kilimo.

Mhandisi Muragili alitoa agizo hilo jana katika kikao cha baraza la madiwani la robo ya kwanza kuanzia Julai-Septemba, 2023/24 kilichofanyika mkoani hapa.

Alisema wakulima wakisajiliwa kwa wakati watapata mbolea na mbegu za ruzuku kwa wakati na hivyo kuwahi msimu wa kilimo kwa kupanda kwa kipindi sahihi na hivyo kupata mazao mengi.

Aidha, Muragili aliwagiza watendaji wa kata kuendelea kukusanya ada za taka ili kurahisisha uendeshaji wa zoezi zima la uwekaji mji katika hali ya usafi wakati wote ili kuepuka magonjwa ya mlipuko hasa katika kipindi hiki cha masika.

Pia, alisisitiza manispaa kuongeza kasi ya ukusanyaji mapato akisema ndiyo mhimili wa halmashauri na kuagiza ukusanyaji wa ushuru wa stendi kuu ya mabasi yaendayo mikoani uwe unafanyika kwa saa 24.

Kadhalika, alisisitiza madiwani wa Manispaa ya Singida kuhakikisha wanasimamia uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la awali na msingi na wale wote watakaojiunga na kidato cha kwanza mwakani waripoti katika shule walizochaguliwa.

## SIDO yawapa neno wahitimu mafunzo ya uokaji bidhaa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la Viwanda Vidogo nchini (SIDO) mkoani Dodoma limetoa wito kwa wahitimu wa mafunzo ya uokaji bidhaa kutumia ujuzi walioupata ili uwasaidie kujikwamua kiuchumi.

Wito huo umetolewa jana na Msimamizi kutoka SIDO, Stephan Ndunguru wakati wa hafla ya kufunga mafunzo hayo jijini hapa.

Mafunzo hayo ya wiki moja yalishirikisha wanafunzi kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini na yametolewa na mtaalamu wa uokaji mikate kutoka nchini Uholanzi.

Ndunguru alisema wahitimu hao wanatakiwa kwenda kuwa mabalozi wazuri katika mikoa wanayotoka, lakini pia wakayatumie kwa vitendo ili kujiinua kiuchumi.

Alisema SIDO kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wamekuwa wakiandaa mafunzo ili kuhakikisha vijana wanapata ujuzi ambao utawasaidia kwenda kujiajiri badala ya kusubiri ajira.

Hivyo, aliwataka vijana kushiriki mafunzo mbalimbali pale yanapotangazwa na SIDO ili kupiga hatua kiuchumi.

Mtaalam wa uokaji mikate kutoka Uholanzi, Bert Steehouder alisema amelazimika kutoa mafunzo kwa vijana ili kuhakikisha washiriki wanafika mbali kwenye uokaji wa bidhaa hizo.

Steehouder alisema ameona juhudi zinazofanywa na washiriki katika mafunzo hayo na kuhimiza kwenda kutumia ujuzi huo kwa vitendo.

Alifafanua zaidi ya kuwa hivi sasa soko la bidhaa Afrika liko vizuri kinachotakiwa ni kufuata utaratibu ikiwamo kusajili biashara ili kutanua wigo wa soko lake.

Akifunga mafunzo, mwakilishi kutoka Wizara ya Viwanda, Festo Katera aliwapongeza SIDO kwa kuandaa mafunzo hayo huku akisema serikali imekuwa ikitoa fursa hiyo ili vijana wawe na ujuzi utakaowasaidia kujiajiri.






Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Alexander Mnyeti (kulia), akikabidhi boti kwa mmoja wa wavuvi wa Ziwa Nyasa katika Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya walionufaika na mkopo wa boti 60 za uvuvi unaotolewa na wizara hiyo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Balozi Marekani aipa siri Tanzania uzalishaji wa chakula

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

IMEELEZWA kuwa Tanzania ikitumia vizuri fursa za kilimo zilizopo inaweza kujitosheleza kwa chakula na ziada kusaidia mataifa mengine ya Afrika pamoja na mataifa mengine duniani yenye shida ya chakula.

Balozi wa Marekani nchini, Michael Battle aliyasema hayo juzi wilayani Mbarali mkoani Mbeya, alipofanya ziara kwenye mashamba ya wakulima wa mboga na matunda ambao wapo chini ya mradi wa Feed The Future Kilimo Tija.

Programu hiyo inafadhiliwa na Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID) inalenga kuwasaidia wakulima kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mazao mbalimbali ili kuisaidia jamii kujitosheleza kwa chakula na kukabiliana na matatizo ya lishe.

Alisema Tanzania ina maeneo mengi yanayofaa kwa kilimo kutokana na hali nzuri ya hewa, ardhi yenye rutuba na maji ya kutosha kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Vilevile alisema uongozi wa Tanzania unaonyesha nia thabiti ya kuendeleza kilimo na kwamba ndiyo sababu inayoisukuma serikali ya Marekani kuendelea kutoa ushirikiano kwa kusaidia maeneo muhimu kwenye sekta hiyo.

"Tanzania ni miongoni mwa mataifa machache Afrika yenye mazingira mazuri ya kilimo, kuna fursa nyingi sana zinazovutia uwekezaji kwenye sekta hii na ndiyo maana sisi tunaamua kufadhili miradi kama hii na tukishirikiana kwa dhati uzalishaji unaweza ukaongezeka zaidi," alisema Battle.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Kanali Dinis Mwila alisema wakulima wamekuwa wakiwezeshwa na taasisi mbalimbali za kifedha kwenye uendelezaji wa sekta hiyo.

Alisema mpaka sasa taasisi hizo zimewawezesha wakulima mikopo yenye thamani ya zaidi ya Dola za Marekani 570,000 ambazo zimewekezwa kwenye maeneo mbalimbali ya uendelezaji wa kilimo kupitia mradi wa kilimo tija.

Aliishukuru Serikali ya Marekani kwa misaada mbalimbali ambayo imekuwa ikiitoa kwa Tanzania kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Mradi wa Kilimo Tija Tanzania, Antonio Coello alisema mradi huo umekuwa na mafanikio mbalimbali kwa jamii ikiwemo kuwasaidia wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao ya bustani.

Alisema katika kipindi ambacho mradi huo umetekelezwa, wajasiriamali wadogo na wa kati waliongeza mauzo ya bidhaa zao na kufikia zaidi ya Sh. bilioni 4.8 na kwamba mauzo hayo ni sawa na ongezeko la asilimia 21 ikilinganishwa na awali.

Hata hivyo baadhi ya wakulima wa Wilaya ya Mbarali walisema moja kati ya matatizo yanayowakabili kwenye uzalishaji wa mazao yao ni upatikanaji wa pembejeo wakieleza kuwa huwa haipatikani kwa wakati na hata bei zimekuwa siyo za kueleweka.

Mmoja wa wakulima hao, Fanuel Vahaye alisema mbali na tatizo hilo la mbolea pia wamekuwa wakikabiliwa na tatizo la mazao yao kuharibika hasa ya kuoza endapo yatakosa soko kwa wakati.

Alisema mazao ya bustani yasipopata soko kwa wakati huwa yanaoza na hivyo kuwasababishia hasara na hivyo akaiomba serikali kuwasaidia kupata masoko ya uhakika.

# Uwanja wa Songwe kuboreshwa, ndege za mizigo kutua

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KAMATI ya Uwezeshaji wa Usafiri wa Anga nchini, imeanzisha mikakati ya kuuboresha Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA) ili kuwezesha ndege kubwa za mizigo kutua na kupaa kwa urahisi.

Kamati hiyo inalenga kuboresha uwanja huo ili kurahisisha usafirishaji wa mazao ya wakulima kwenda kwenye masoko mbalimbali ya kimataifa hasa mazao ya mboga na matunda.

Akizungumza wakati wa kikao cha kamati hiyo kilichofanyika jijini Mbeya, Mwenyekiti wa kamati hiyo, Daniel Malanga alisema wameamua kuanzisha mikakati hiyo baada ya kubaini ongezeko kubwa la abiria na mizigo inayosafirishwa kwenye uwanja huo.

Alisema katika Mkoa wa Mbeya kumekuwa na kasi kubwa ya ongezeko la abiria wa ndani na nje ya nchi wanaotumia uwanja huo ambao alisema unasaidia mataifa mbalimbali ya Ukanda wa SADC.

"Pamoja na kwamba kumekuwepo na ongezeko la mizigo ya wakulima inayosafirishwa kupitia uwanja huu lakini kuna tatizo la baadhi ya mazao ya wakulima kuoza yakiwa bado hayajasafirishwa na hivyo kikao hiki kitakuja na mikakati ya kutatua tatizo hilo," alisema Malanga.

Hivyo, aliwataka wananchi wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kuendelea kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali kwa maelezo kuwa kwa sasa serikali imeendelea na mikakati ya kuboresha miundombinu ya usafiri na usafirishaji.

# Watu 163 mbaroni tuhuma wizi pikipiki, bajaji

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WATU 163 wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani hapa kwa tuhuma mbalimbali za uhalifu ikiwemo wizi wa bajaji na pikipiki.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Mahamoud Banga aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Banga alisema watu hao walikamatwa kufuatia msako uliofanywa na kuanzia Septemba moja mpaka Oktoba 31 mwaka huu.

Alisema licha ya kukamatwa kwa watuhumiwa hao pia walifanikisha kukamata bajaji, pikipiki na vifaa vingine.

"Tumekamata bajaji zipatazo nane, pikipiki tatu, matairi ya bajaji sita, dizeli lita 328, bangi gramu 200, simu pamoja televisheni," alisema.

Hata hivyo alitoa wito kwa madereva wa bajaji mkoani Njombe kuhakikisha kuwa wanawafahamu abiria wanaowabeba na mazingira wanayoenda ili kuepuka uporaji wa bajaji hizo.

"Kumekuwa na tabia ya watu kukodiwa na kupelekwa maeneo hatarishi ambayo wanakwenda kunyang'anywa bajaji lakini jeshi limeendelea kufanya doria na kuwasaka wanaojihusisha na uporaji wa bajaji," alisema Banga.

Wakati huo huo Jeshi la Polisi mkoani Njombe linamshililia Stephano Mng'ong'o (55) baada ya kukutwa na silaha moja aina ya gobole ambayo alikuwa anaimiliki kinyume cha sheria.

Mwenyekiti wa madereva wa bajaji Wilaya ya Njombe, Richard Luganga alisema wizi wa bajaji umesababisha mgongano mkubwa kati ya madereva na wamiliki wa bajaji mkoani Njombe.

"Kwa madereva imezua taharuki baada ya kuona vile vyombo ambavyo wao wanatumia kutafutia riziki vinatoweka katika mazingira ambayo hayaeleweki," alisema Luganga.

Mmoja ya madereva wa bajaji mjini Njombe, Geofrey Mwinuka alisema bajaji zilizo nyingi zinaibiwa muda wa kuanzia saa tano mpaka saa nane usiku.

Alisema: "Bajaji nyingi zinaibiwa sehemu tunayopaki hasa sehemu ambazo siyo salama kwani kwenye ulinzi mzuri bajaji haziibiwi".





Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimwapisha Khadija Shamte Mzee kuwa Jaji wa Mahakama Kuu Zanzibar, hafla hiyo iliyofanyika ukumbi wa Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Serikali yakusanya mil.91/- makosa barabarani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imefanikiwa kukusanya tozo ya shilingi milioni 91.5 zitokanazo na makosa ya barabarani kwa kipindi cha Oktoba mwaka huu.

Tozo hizo zimepatikana kutoka katika makosa 2,550 yaliyofikishwa mahakamani na wahusika kutozwa faini.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Ramla Hassan Pandu, alitoa taarifa hiyo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari akisema ajali 16 zimeripotiwa katika kipindi hicho.

Alisema waathirika waliojeruhiwa katika ajali hizo ni 24 na Wilaya ya Kati Unguja ndiyo inayoongoza kwa kuwa na ajali nyingi na makosa mengi ya barabarani ikilinganishwa na wilaya zingine.

Ramla alisema waathirika wa ajali waliofariki katika kipindi hicho wameongezeka kwa asilimia 7.7 kufikia waathirika 14 waliofariki ikilinganishwa na kipindi cha Septemba ambao ni 13.

Aidha, alisema waathirika wengi wa ajili hizo ni abiria na waliofariki ni waenda kwa miguu ambao walikuwa nane kati ya 16 waliofariki huku waendesha pikipiki na baskeli ni wanne na maderva wa magari ni watatu.

Alisema chanzo cha ajali hizo ni mwendokas i wa madereva na uzembe na chanzo cha makosa ya barabarani yaliyoripotiwa ni kutokufuata miongozo na kanuni za usalama barabarani.

Hata hivyo alisema idadi ya makosa ya barabarani yamepungua kwa kipindi cha Oktoba kwa asilimia 10.7 ambayo yalikuwa 3,389 ikilinganishwa na kipindi cha Septemba mwaka huu ambayo yalikuwa 3,797.

Ofisa wa leseni kutoka Idara ya Usafiri na Leseni, Nassor Mwinyi, aliwataka wazazi, walezi na jamii kutowakabidhi watoto walio chini ya umri wa miaka 18 kuendesha vyombo vya moto ambao wengi wao wamekuwa wakipata ajali.

Alisema ni kosa kisheria mtoto chini ya miaka 18 kuendesha chombo cha moto, lakini pia ni kosa kwa mzazi au mtu yoyote kumkabidhi mtoto chombo cha moto na faini yake kwa mzazi ni Dola za Marekani 50.

Aidha, aliitaka jamii kuacha kuwakabidhi vyombo vyao vya moto watu wengine ambao hawana leseni kwa sababu imebainika maderva wengi wanaopata ajali vyombo huwa sio vyao.

Sajeti Ali Abdallah Pandu, kutoka kitengo cha usalama barabarani makao makuu ya Jeshi la Polisi Zanzibar, aliwataka madereva kuwa na tahadhari wanapokuwa barabarani hasa kipindi cha mvua.

Aidha, alitoa tahadhari kwa miliki wa vyombo vya moto wanapopeleka vyombo vyao kusafishwa katika vituo cha kuoshea magari kutoacha funguo, pamoja na kuhakikisha wanasimamia hadi muhusika anapoliza kuosha.

# Wadau wa nishati wakutana kujadili matatizo yanayowasibu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WADAU wa maendeleo kutoka nchi mbalimbali katika sekta ya nishati wamekutana visiwani Zanzibar kujadiliana matatizo yanayoikabili Zanzibar katika sekta ya nishati, pamoja na kupata ufumbuzi.

Akifungua mkutano huo jana Naibu Waziri wa Maji na Nishati, Shaaban Ali Othman, alisema Zanzibar inahitaji miradi mikubwa ya uzalishaji wa nishati ya umeme kwa sababu inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo umeme mdogo na kukatika kwa umeme mara kwa mara.

Alisema Zanzibar inatekeleza miradi mikubwa ya maendeleo, hivyo inahitaji umeme wa uhakika, akisema wadau hao wataisadia Zanzibar katika upatikanaji wa fedha na vifaa vya kuzalisha umeme wa kutosha na wa ziada.

Alisema Serikali ya Zanzibar imeshasaini mikataba miwili mikubwa ya uzalishaji wa umeme mbadala ikiwemo umeme ya jua na upepo.

Alisema miononi mwa kampuni hizo zilizotiliana saini ni Generation Capital ambayo itaanza na uzalishaji wa megawati 30 za umeme mbadala kwa Unguja na kampuni ya ISR ya nchini ambayo itazalisha megawati 15 kisiwani Pemba.

Aidha, alisema kuwa pia Zanzibar inatekeleza mradi wa ZESTA ambao unazalisha umeme wa jua megawati 18 eneo la Makunduchi Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema uwekezaji katika sekta ya umeme ni mkubwa unaotekelezwa ili kutoa huduma ya maji, nishati na madini kwa wananchi katika kiwango bora na ndani ya muda mfupi.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, John Joseph Kilangi, alisema lengo la kushirikisha wadau hao ni kusaidia kusambaza nishati ya umeme mjini na vijijini na kuhakikisha kuwa Zanzibar ina umeme wa uhakika.

# Viongozi shehia, wadi watakiwa kuzingatia takwimu za sensa

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

VIONGOZI wa ngazi ya shehia na wadi wametakiwa kuzifanyia kazi takwimu za matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 katika kuhakikisha malengo ya serikali yanatimia.

Wito huo umetolewa juzi na Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi Unguja, Idrissa Kitwana Mustafa, alipokuwa akifungua kikao cha usambazaji na matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi 2022 ngazi ya mkoa, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Alisema, matokeo ya sensa yamefanikiwa kwa kiwango kikubwa kuonyesha hali ilivyo, hivyo masheha na watendaji wakuu wa mikoa, wilaya na makatibu tawala wana dhima ya kuhakikisha wanazifanyia kazi takwimu hizo kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Alisema: "Kwa kuzitumia takwimu hizo tunaweza kupanga bajeti na mipango ambayo itakuwa jumuishi kwa ajili ya maendeleo endelevu," alisema.

Pia alisema matokeo ya sensa yamekuwa dira sahihi ya mipango ya maendeleo katika kubuni na kuandaa sera mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa mipango ya kijamii, ikiwemo afya, elimu na miundombinu jumuishi.

Aidha, aliwapongeza masheha na watendaji ngazi ya shehia kwa kufanya kazi nzuri kubwa ya kuwahamasisha wananchi kushiriki katika Sensa ya Watu na Makazi na hivyo kusababisha kufanikiwa kwa asilimia 100.

Akiwasilisha baadhi ya matokeo kwa kutumia ramani, Mtakwimu Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Nassir Hamad Salum, alisema viashiria vilivyopo kwa kila halmashauri na shehia vimeonyesha namna ya uhalisia na kuhitajika kufanyiwa kazi.

Mada nyengine zilizowasilishwa na OCGS ni matokeo muhimu ya baadhi ya viashiria vya kiuchumi, kijamii na mazingira vitokanavyo na Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Salum Kassim Ali, alisema imani yake kwamba takwimu hizo zitatumika katika kupanga mipango ya taifa kuanzia ngazi ya shehia, wilaya na mkoa katika kufikisha maendeleo ya wananchi na serikali kuu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**SUZAN KUNDI JILALA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA PASSO yenye usajili namba T 390 DVY, CHASSIS NAMBA: KGC100229514 na ENGINE NAMBA: 1KK0717534. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA:**

**PHQ/DAR/KIN/36824/2023**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**DOUGLAS DUNCAN SIMBEYE**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya RANGE ROVER yenye jina la umiliki SWALA SAFARIS LIMITED yenye usajili namba: T 199 ADC, yenye chassis namba : 35501250A na ENGINE NAMBA: 25D1357B. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA:**

**PHQ/ARU/ARU/7132/2023**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**PRAYGOD JACKSON LEMA**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA LANDCRUISER, yenye jina la umiliki TOP GUIDES SAFARIS LIMITED, namba ya usajili T 591 CKZ, CHASSIS NAMBA: JTEBB71J804000819 na ENGINE NAMBA: 1HZ0637131. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA:**

**PHQ/ARU/ARU/7132/2023**

## KUPOTELEWA NYARAKA UMILIKI KIWANJA

**DICKSON JOSEPH MSELUKA**

Anatangaza kupotelewa na Nyaraka ya Umiliki wa Kiwanja namba 238A Kitalu 'HH' Kilichopo Ndala Manispaa ya Shinyanga.

Kwa yeyote atakaiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Dickson kwa simu namba 0713-783555.

Taarifa ya Polisi

**RB:PHQ/SHI/SHI/1122/2023**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**FRANSISCA EMANUEL MAYATA**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya boxer yenye usajili namba MC 551 CSR .

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .

Polisi Taafifa :

**PHQ/DAR/ILA/385775/2023**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**JAMILA ASHERY ISDORY**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya SUZUKI SWIFT yenye usajili namba T 170 BJY, CHASSIS NAMBA: HT51S744990 na ENGINE NAMBA: M13A12669946. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA :**

**PHQ/ARU/ARU/7132/2023**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA)**
**Mahakama ya Mwanzo ARUSHA –MJINI**
**Wilaya ya ARUSHA**
**MADAI NAMBARI 367/2023**
**Mdai SHARIFA ABDUL KIRIWE**
**Amdai**
**Mdaiwa GODLISTEN SWAI**

**Kwa . GODLISTEN SWAI**
**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yako kwamba (Eleza hapa habari za Madai)**

**UNAAMRIWA NA MAHAKAMA HII UFIKE BILA KUKOSA KUJIBU DAI LA T.SHS 10,8000,000/=**

Kwa hiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria Mahakama hii siku ya JUMATATU 20/11/2023 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo, ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hili, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 09/11/2023

..............................................

**Hakimu /Hakimu mkazi Mahakama ya Mwanzo.**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 143 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**ESTHER BENEDICT MTAMBUU**
**Of Makole within Dodoma City**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATIONFOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**FURAHA MTAMBUU and JOYCE MTAMBUU**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES Gn.369 OF 1963)**

ALL PERSONS Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Admiration is made to the above named petitioner. Objections to the grant should be filed on or before the 06th Day of DECEMBER, 2023.

Dated at Dodoma this 15th day of NOVEMBER, 2023

..............................................

**RESIDENT MAGISTRATE**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Moshi**
**Kituo cha Moshi Mjini Mkoa Kilimanjaro**
**Shauri la Madai 227 , 2023.**
**Jina la Mdai Antipas Beda Marandu.**
**Jina la Mdaiwa Florenko Emmanuel . 2. Emmanuel Ndekio.**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**Kwa: Florenko Emmanuel**
**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta /Wameleta madai yao kwamba (eleza hapa habari za Madai )**

**Mdai anadai pikipiki yake yenye thamani ya tsh 1,800,000/=pamoja na marejesho ya 1,120,000/=hivyo fika mahakamani kujibu madai haya.**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 29 mwezi 11 mwaka 2023 saa 03:00 asubuhi kwa mujibu wa maombi hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashaidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya w ewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 16 mwezi 11 Mwaka 2023

..............................................

**HAKIMU**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......25/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: ABDALLAH ALLY DIHIGO wa K/NDEGE**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA RASHID SAID ABDALLAH**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 20 Mwezi 11 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 09 mwezi 11 mwaka 2023

---

**OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.**

**Mob: +255 - 0677020701**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**Website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Afrika Kusini yaishtaki Israel ICC

**PRETORIA, Afrika Kusini**

KUTOKANA na hali mbaya ya kibinadamu kutishia kuangamiza Ukanda wa Gaza, serikali ya Afrika Kusini imeishtaki Israel katika Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) ikitaka kufanyika uchunguzi wa uhalifu wa kivita.

Rais wa nchi hiyo, Cyril Ramaphosa alisema hatua hiyo imechukuliwa kutokana na jukumu la kidunia katika mzozo unaoendelea huko Gaza.

"Afrika Kusini, kama nchi nyingine nyingi duniani, tumeona inafaa kuishtaki serikali ya Israel kwenye Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu. Tumetuma rufaa kwa sababu tunaamini kuwa uhalifu wa kivita unafanywa huko," alisema Rais Ramaphosa.

Hata hivyo, hakufichua nchi nyingine zilizoshtaki Israel ICC.

Aliongeza kwamba Afrika Kusini hawakuunga mkono shambulio la awali la Hamas dhidi ya Israel lakini wanapinga hatua zinazofanywa na Israel katika eneo hilo ambazo wanaamini uchunguzi unastahili kufanywa na ICC".

ICC ni chombo cha kimataifa ambacho kina kazi ya kuchunguza na kuwahukumu watu binafsi wanaotuhumiwa kufanya uhalifu unaotia wasiwasi jumuiya ya kimataifa, kama uhalifu wa kivita au mauaji ya halaiki.

Afrika Kusini imekuwa ikiwaunga mkono Wapalestina katika mzozo unaoendelea na Israel.

Viongozi kadhaa wa nchi hiyo wamewaunga mkono hadharani Wapalestina na pia kumekuwa na maandamano ya kuunga mkono mitaani.

Katika hatua nyingine, Rais wa Marekani Joe Biden amesema ana matumaini kidogo ya kuwepo kwa mpango wa kuwakomboa zaidi ya watu 200 wanaoshikiliwa mateka Gaza.

Kiongozi huyo aliwaambia waandishi wa habari mjini California kwamba hakutaka kuzungumza kabla ya wakati, lakini Marekani imeona ushirikiano mkubwa kutoka kwa Qatar, ambayo imekuwa ikiongoza mazungumzo yanayoendelea kati ya Israel na Hamas.

Akizungumzia operesheni ya hivi karibuni ya Israel katika hospitali kubwa Ukanda wa Gaza ya Al-Shifa, kiongozi huyo alisema Hamas ilifanya uhalifu wa kivita kwa kuwa na kituo chini ya jengo hilo.

Awali Israel ilionyesha kile inachodai kuwa ni ushahidi wa silaha na vifaa vingine vya Hamas ambavyo vilipatikana ndani ya hospitali hiyo.

Hata hivyo, Hamas inakanusha kuwa inatumia vituo vya matibabu kama ngome ya harakati zake za kijeshi dhidi ya Israel.

Rais Biden alisema Marekani imeitaka Israel kuwa makini , kuhakikisha kuwa raia wanakuwa salama wakati wa kuzisaka ngome za Hamas.

Wakati huo huo, Maofisa sita wa polisi wamejeruhiwa baada ya waandamanaji kukabiliana na vikosi vya usalama nje ya ofisi za Kamati ya Kitaifa ya Kidemokrasia ya Marekani (DNC) iliyoko Washington.

Askari waliovalia zana za kudhibiti ghasia walitumia pilipili ili kuwatawanya waandamanaji hao waliokuwa wakitaka kusitishwa kwa shughuli za kijeshi za Israel ndani ya Gaza.

Mbunge wa California Brad Sherman alikuwa miongoni mwa waliolazimika kuhamishwa kutoka ndani ya ofisi hizo.

"Waandamanaji walikua na vurugu, wakiwapulizia pilipili polisi na kujaribu kuingia ndani ya jengo hilo," aliandika kwenye mtandao wa kijamii.

Upekuzi Al Shifa

Shirika la Habari la Associated Press limearifu kwamba msako mkali unaendelea kufanywa na wanajeshi wa Israel ndani ya hospitali ya Al Shafa.

Ilisema wanajeshi hao waliamuru vijana wote mabarobaro kujisalimisha, wakatolewa nje ya majengo ya hospitali na kufanyiwa upekuzi mkali na wengine wakiwa hawana nguo.

Mwandishi habari wa shirika moja la kimataifa aliye miongoni mwa watu waliokwama kwenye hospitali hiyo, alisema vikosi vya Israel vilifanya upekuzi kwenye kila chumba.

Jeshi ladai kupata silaha

Msako huo ulimalizika majira ya jioni kwa taarifa ya jeshi la Israel kueleza askari wake wamekuta silaha, nyaraka za ujasusi na vifaa vya kijeshi ndani ya hospitali.

Walidai wamevikuta vifaa vya mawasiliano vyenye kuashiria kwamba eneo hilo ndiyo yalikuwa makao makuu ya mawasiliano ya kundi la Hamas.

Jeshi la Israel limechapisha taarifa zinazoonyesha bunduki, maguruneti na vifaa vingine ambavyo inadai imevikuta ndani ya hospitali.

Wizara ya Afya ya Ukanda wa Gaza imekanusha madai hayo ikisema vikosi vya Israel havikukuta vifaa vyovyote vya kijeshi wala silaha ndani ya hospitali.

Wizara hiyo ya Afya imewatuhumu wanajeshi wa Israel kwa kuharibu vifaa vya matibabu inavyosema havipatikani ndani ya ukanda wa Gaza.

**BBC**



Vifaru vya jeshi la Israel vikiwa ndani ya Ukanda wa Gaza vikifanya mashambulizi.**PICHA: IDF**

## Uingereza yasisitiza wahamiaji lazima wapelekwe Rwanda

**LONDON, Uingereza**

SERIKALI ya Uingereza imesisitiza bado itaendelea na mpango wake wa kuwapeleka baadhi ya wahamiaji haramu nchini Rwanda.

Waziri Mkuu wa Uingereza Rishi Sunak, ambaye aliahidi kuwazuia wahamiaji kufika Uingereza kwa kutumia boti ndogo kupitia ujia wa bahari wa Uingereza, alisema uamuzi wa mahakama wa kuzuia haukuwa matokeo waliyoyataka.

Hata hivyo, aliapa kuendelea na mpango huo na kupeleka ndege za kwanza zilizobeba wahamiaji hao kuelekea Rwanda kufikia msimu ujao wa masika.

Sunak alisema mahakama imethibitisha kuwa kanuni ya kuwahamisha waomba hifadhi kwa taifa la tatu ni halali hata kama iliamua kuwa Rwanda sio salama.

Sunak alipendekeza kuwa ikiwa changamoto za kisheria kwenye mpango huo zitaendelea, yuko tayari kuzingatia kujiondoa katika mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu.

Hatua hiyo huenda ikaleta upinzani na ukosoaji wa kimataifa.

## Marekani, China zakubali kurejesha mawasiliano

**WASHINGTON, Marekani**

VIONGOZI wa mataifa ya Marekani na China wamekubaliana kurejesha mawasiliano ya kijeshi kati ya nchi hizo mbili.

Rais Joe Biden wa Marekani na Xi Jinping wa China walikubaliana katika mkutano wao wa kwanza uliofanyika nchini Marekani.

Viongozi hao walisalimiana kwa mikono kabla ya kufanya mazungumzo ya saa nne yaliyojikita katika kuzuia mivutano inayoongezeka kati ya dola hizo mbili kubwa duniani kuepuka kuwa mzozo kamili.

Walikubaliana kuwa China itadhibiti uzalishaji wa dawa za kulevya za opioid ambazo zimekuwa janga nchini Marekani.

Rais Xi alisema China iko tayari kushirikiana na Marekani.

Hata hivyo Rais Xi na Biden waliendelea kutofautiana kuhusu suala la Taiwan, huku rais wa China akimtaka mwenzake wa Marekani kukoma kukipa kisiwa hicho silaha za kivita na kwamba suala la kuungana tena halizuiliki.

**DW**

## Papa Francis apiga marufuku waumini kujiunga Freemasons

**VATIKAN, ROMA**

KANISA katoliki limethibitisha kwamba Papa Francis amepiga marufuku waumini wake kujiunga na kuwa wanachama wa muungano wa Freemasons.

Katika waraka mpya uliotiwa saini na Papa Francis ulisema mafundisho ya Kikatoliki na uanachama wa Freemason hayawezi kutangamana au hayapatani .

Barua hiyo iliyotolewa na ofisi ya mafundisho ya Vatikani ilinukuu tamko hilo lililotolewa miaka arobaini iliyopita, likisema kwamba wakatoliki waliojiunga na chama cha freemason hawaruhusiwi kushiriki katika ekaristi takatifu.

Uamuzi huo wa Papa Francis unaonekana kumjibu Askofu kutoka Ufilipino ambaye alionyesha wasiwasi wake juu ya kuongezeka kwa idadi ya Wakatoliki katika dayosisi yake wanaojiunga na vyama vya freemason.

# AZAM YATENGA BAJETI USAJILI DIRISHA DOGO

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Azam FC imesema tayari imeshatenga fungu la bajeti kwa ajili ya usajili wa dirisha dogo utakaoanza Desemba 16 mwaka huu huku ikilenga wachezaji watakaokwenda kukiongezea nguvu kikosi chao.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Thabit Zacharia 'Zaka' amesema jana kuwa, timu kubwa kama Azam itakuwa ni stori kubwa kwenye vyombo vya habari kama dirisha dogo litapita bila kufanya usajili.

Pamoja na hayo yote amesema jukumu lote wanamuachia Kocha wao Mkuu, Youssouph Dabo, ambaye ndiye atakuwa na mamlaka ya mwisho juu ya mchezaji anayemtaka.

"Usajili ni muhimu, timu kubwa kusajili ndiyo maisha yake ndiyo chakula chake, isiposajili ndiyo inakuja stori kwamba timu fulani haijasajili, kama hatutosajili ni lazima tutatengeneza habari kubwa kwenye vyombo vya habari, ila naweza kusema tu tutafanya usajili kuboresha sehemu chache, kuna sehemu zinahitaji kuongeza watu kwa sababu wengine wanaumia hivyo mapungufu lazima yataonekana, kwa hiyo lazima tutafanya usajili wa maboresho," alisema Zaka.

Aidha, alisema msimu huu wanauhitaji ubingwa kwa udi na uvumba na mpaka sasa wapo nafasi ya pili kwa pointi 19, hivyo wataongeza wachezaji kwa ajili ya kuwasaidia waliopo.

"Najua yote haya inategemea pia matakwa ya mwalimu, anaweza akasema hawa wanatosha, lakini tunamuachia yeye maamuzi yote, kama akiangalia akaona kuna umuhimu kuongeza nguvu kazini tutafanya hivyo kwa sababu tayari tumetenga bajeti ya usajili, akisema anataka kuongeza mtu au watu atasaidiwa tu kwa sababu klabu tayari ina bajeti ya usajili," alisema Zaka.

Alisema timu yao bado ipo kwenye mbio za ubingwa na kwamba kuna michezo mingi ya Ligi Kuu mbele yao hivyo kama watachanga karata zao vizuri kwenye michezo hiyo nafasi ya ubingwa bado wanayo.



Watoto wakicheza mpira wa kikapu bila viatu kama walivyokutwa jana kwenye viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba Queens wanautaka ubingwa

**Na Saada Akida**

KOCHA msaidizi wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi' amesema wameanza maandalizi mapema kwa ajili ya msimu mpya wa ligi kuu ya wanawake Tanzania Bara huku lengo likiwa kutwaa ubingwa na kurejesha heshima yao.

Simba imepoteza ubingwa wake msimu huu uliochukuliwa na JKT Queens na sasa timu hizo zinajiandaa na msimu mpya.

Kikosi cha Simba Queens kiko chini ya Kocha Juma Mgunda akisaidiwa na Mgosi na kinaendelea na maandalizi yake kuelekea kwenye michezo ya Ngao ya Jamii itakayofanyika Desemba 8-12 kabla ya Ligi Kuu kuanza kati ya Desemba 15 na 16.

Akizungumza na Nipashe jana, Mgosi alisema maandalizi yanaendelea vizuri kwa wachezaji ambao hawako kwenye majukumu ya timu za Taifa na wale waliopo kwenye timu za taifa watajiunga moja kwa moja na timu hiyo mara baada ya kumaliza majukumu yao.

Alisema kikosi chake kilichoanza maandalizi kinawako wachezaji sita ambao wapo kwenye majukumu ya timu za taifa.

"Kazi kubwa imebaki kuwaandaa wachezaji kimbinu na ufundi, usajili umefanyika vizuri, kukosa ubingwa msimu uliopita kumeleta huzuni kwa wachezaji, lakini hii imeongeza morali mazoezini na kila mchezaji anaonekana kuwa tayari kurejesha heshima ya timu," alisema Mgosi.

Alisema Wanasimba watulie kwani wamepania walichokipoteza msimu uliopita watakirejesha kwenye msimu mpya.

"Kwa sasa mazoezi tumefikia asilimia 60 na kila siku zinavyozidi kwenda tunakuwa bora zaidi kabla ya mchezo wetu wa Ngao ya Jamii kuanza tutakuwa tumimarika zaidi," alisema Mgosi.

Aliongeza kuwa ili kuwa mabingwa lazima kuhakikisha wanaanza vizuri kwa kuchukua taji la ngao ya Jamii ambayo itaongeza morali katika kulifukuzia taji la Ligi Kuu. Kwa upande wa wachezaji, mchezaji mwandamizi kwenye kikosi hicho, Fatuma Issa ' Fetty Dancer ', alisema msimu huu wamekuja kivingine kwa kupambana kusaka matokeo mazuri katika mashindano yaliyopo mbele yao.

"Msimu uliopita tulipoteza ubingwa, tukajiuliza tumekosea wapi , sasa tumerejea kazini na tuko tayari kukutana na timu yoyote katika mchezo wa Ngao ya Jamii na Ligi pia," alisema Fetty.

# Zanzibar U-18 wapania CECAFA

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA wa timu ya taifa ya soka ya Zanzibar kwa vijana wenye umri chini ya miaka 18, Ali Mohamed Ameir, amesema wanataka kufanya vizuri kwenye mashindano ya Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA).

Ameir amesema lengo hilo ndio sababu ya kuanza maandalizi yao mapema kuelekea kwenye mashindano hayo yatakayoanza mwishoni mwa mwezi huu nchini Kenya.

Akizungumza na gazeti hili viswani hapa, Ameir alisema tayari ameshafanya mchujo na kupata wachezaji 22 ambao ndio watakaosafiri na timu hiyo kuipeperusha bendera ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla katika mashindano hayo.

"Tupo kwenye maandalizi makali, tuna ratiba ya mazoezi ya mara mbili kwa siku ambayo tunafanya kwenye uwanja wa Mau, kikubwa tunataka kufanya vizuri, hatutaki kuwa washiriki tu," alisema Ameir.

Alisema katika maandalizi hayo tayari ameshacheza mechi za kirafiki michezo kadhaa na timu za Ligi kuu ya Zanzibar na zile za Kanda.

Alisema kupitia michezo hiyo ya kirafiki wachezaji wameonyesha viwango vizuri na kufuata maelekezo ya mwalimu na hiyo inampa matumaini ya kwenda kufanya vizuri katika michuano hiyo.

"Tunaendelea na mazoezi yetu kueleke michuano ya CECAFA, lengo letu kama wenzetu tu kuhakikisha tunafanya vizuri katika michuano hiyo ambayo inawakutanisha vijana, siku zote michuano ya Vijana inakuwa migumu mno kwakuwa inawashirikisha wachezaji ambao bado wana hamu Kubwa ya kucheza soka na hasa katika kuitumikia timu yao ya Taifa,"alisema Ameir.

Aidha alisema kuwa kulingana naratiba za mechi za CECAFA kuwepo mechi za mchana, ameweka kwenye programu yake ratiba ya mazoezi ya mchana ili wachezaji wake wazoee mazingira ya kucheza mechi muda huo.

"Kwa mujibu wa ratiba ya michuano ya CECAFA ilivyo huwa kuna michezo za saa saba mchana ambapo jua huwa kali, sasa ni lazima na sisi katika kipindi hiki tupate nafasi hiyo ya kufanya mazoezi mchana wakati wa jua kali walau kwa wiki moja kabla ya safari lakini hali hewa ya mvua kwetu inatukwamisha"Alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### NEWCASTLE YAMTAKA TORRES

KLABU ya Newcastle United inamtaka mshambuliaji wa Hispania, Ferran Torres, ambaye Barcelona wanajiandaa kumuuza baada ya mchezaji huyo wa zamani wa Manchester City mwenye umri wa miaka 23 kushindwa kufikia matarajio ya klabu hiyo ya La-Liga. **(Fichajes)**

### DAVIES AWINDWA ENGLAND

CHELSEA, Liverpool na Manchester City zinamwania beki wa Bayern Munich, Alphonso Davies mwenye umri wa miaka 23, lakini wanaamini mchezaji huyo anatamani sana kujiunga Real Madrid. **(90min)**

### TAHA ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inatafakari uwezekano wa kumnunua mlinzi wa Ujerumani na Bayer Leverkusen Jonathan Tah mwenye umri wa miaka 27 Januari mwakani. **(Sun)**

### SANCHO NA MAN

MANCHESTER United imepanga kukataa kumruhusu Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 23 kuondoka kwa bei nafuu katika dirisha la uhamisho la Januari - licha ya kocha Erik ten Hag kutaka kumwondoa winga huyo wa England. **(Mirror)**

### MOSCARDO AWA LULU ENGLAND

CHELSEA ipo tayari kushindana na Arsenal na Liverpool kwa ajili ya kumnunua kiungo wa kati wa Corinthians mwenye umri wa miaka 18 kutoka Amerika Kusini, Gabriel Moscardo, ambaye thamani yake ni pauni milioni 26. **(Standard)**

***

### WILSON NJE WIKI SITA

MSHAMBULIAJI wa Newcastle United na England, Callum Wilson mwenye umri wa miaka 31 atakuwa nje ya uwanja kwa karibu wiki sita kutokana na jeraha la misuli ya paja, huku mchezaji mwenzake Sven Botman mwenye miaka 23 akitarajiwa kuwa nje kwa muda mrefu zaidi kwa sababu ya tatizo la goti. **(Telegraph)**

### UNITED YAKOMAA NA FERGUSON

KLABU ya Manchester United itaendelea kumfuatilia mshambuliaji wa Brighton, Evan Ferguson mwenye umri wa miaka 19 licha ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Jamhuri ya Ireland hivi karibuni kusaini mkataba mpya na Seagulls hao. **(Football Insider)**

### SCHRODER KUONDOKA

MKURUGENZI wa RB Leipzig, Rouven Schroder amefungua mlango kwa mshambuliaji wa zamani wa Chelsea, Timo Werner mwenye umri wa miaka 27 kuondoka katika klabu hiyo, huku Mjerumani huyo akiwa ameanza mechi mbili pekee msimu huu. **(Standard)**

### UNITED MASHAKA MATUPU

KUNA mashaka kuhusu mustakabali wa mkurugenzi wa soka wa Manchester United John Murtough na mkurugenzi wa uendeshaji wa soka, David Harrison baada ya tangazo kwamba mtendaji mkuu Richard Arnold ataondoka katika klabu hiyo. **(Mirror)**

### EZE KUONGEZEWA

MSHAMBULIAJI wa England, Eberechi Eze mwenye umri wa miaka 25, anakaribia kukubali mkataba mpya utakaomfanya alipwe pauni 100,000 kwa wiki katika klabu ya Crystal Palace baada ya kuafikiana kimsingi na klabu hiyo. **(Mail)**

## DOND... SOKA MAC... LAYA




# MAN UNITED HAITAKUBALI OFA NDOGO KWA SANCHO

●●●United itaanza kusikiliza ofa kwa ajili ya fowadi huyo wa England baada ya...

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United haitamruhusu Jadon Sancho kuondoka kwa bei nafuu kama ataondoka Januari, kwa mujibu wa ESPN.

United itasikiliza ofa kwa ajili ya fowadi huyo wa England huku akiendelea kuondolewa kwenye kikosi cha kwanza baada ya mabishano yake ya hadharani na Kocha Erik ten Hag.

Sancho, ambaye hajacheza tangu Agosti anazivutia timu za Juventus na Borussia Dortmund lakini United wanataka kupunguza athari za kifedha za kuondoka kwake iwezekanavyo.

Chanzo kimoja kimeiambia ESPN kwamba Man United wanafahamu kuwa klabu pinzani pia zitajaribu kuchukua fursa ya hali ya Sancho pale Old Trafford na watamtaka kwa mkopo mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 huku wakiitaka United kulipa sehemu kubwa ya mshahara wake wa pauni 300,00 kwa wiki.

United haijakataa kukubali mkataba wa muda mfupi lakini ingependa mchango mkubwa katika mshahara wake na kwa hakika kuwa na ada ya mkopo.

Sancho, ambaye aliwasili kwa mkataba wa pauni milioni 73 kutoka Borussia Dortmund mwaka 2021 yuko chini ya mkataba hadi mwaka 2026 na chaguo la kuongeza mwaka mwingine.

Ten Hag amemtaka Sancho aombe radhi kwa kupinga hadharani sababu za kuachwa kwenye kichapo cha 3-1 kutoka kwa Arsenal Septemba mwaka huu, kitu ambacho hadi sasa amekataa kufanya.

Wakuu wa United akiwamo Mkurugenzi wa Soka, John Murtough, wamemuunga mkono Ten Hag na kulingana na chanzo, Mholanzi huyo hana uwezekano wa kulegeza msimamo wake iwapo ataombwa kukagua hali hiyo na mwanahisa anayekuja Sir Jim Ratcliffe na timu yake.

Ununuzi wa Ratcliffe wa hisa asilimia 25 kwa ada ya karibu pauni bilioni 1.3 unatarajiwa kukamilishwa mara moja.

Hata hivyo, chanzo kiliiambia ESPN kwamba Ten Hag ataendelea kumtaka Sancho aombe msamaha kwa faragha na hadharani kabla ya kuzingatia ikiwa kuna njia yoyote ya kurudi kwake United.

# MAN CITY YAWEKA REKODI YA MAPATO ENGLAND

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester City imeweka rekodi ya mapato ya Ligi Kuu England kufikia pauni milioni 712.8 kwa mwaka wa fedha wa msimu wa 2022-23.

Hii inazidi rekodi ya pauni milioni 648.4 iliyowekwa mwezi uliopita na Manchester United na ni ongezeko la pauni milioni 99.8 ikilinganishwa na mwaka uliopita.

Faida ya City ya pauni milioni 80.4 imepanda kutoka rekodi ya mwaka jana ya klabu hiyo iliyokuwa pauni milioni 41.7.

Takwimu hizo zimekuja baada ya msimu uliopita kushinda mataji matatu na kuwa timu ya pili England kufanya hivyo baada ya Manchester United mwaka 1999 ilipotwaa Ligi Kuu, Kombe la FA na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Baada ya ushindi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na kukamilika kwa 'mataji matatu' swali ambalo nilikuwa nikiulizwa mara nyingi, lilikuwa 'je, unaongozaje hapo?

"Mafanikio ya leo yanamaanisha uwekezaji zaidi kwa kesho. Pia mafanikio yetu ya pamoja yananipa imani kubwa kwamba kwa pamoja tunaweza kutimiza hata zaidi katika miaka ijayo," alisema Mwenyekiti wa Man City, Khaldoon al-Mubarak.

Taarifa ya fedha ya klabu inaonesha kuongezeka kwa vyanzo vyote vikuu vya mapato ambapo mapato ya matangazo yaliongezeka kwa asilimia 20.2 sawa na pauni milioni 299.4.

City imesema hiyo ilitokana na mafanikio yao katika Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la FA.

Klabu hiyo ilipata faida ya pauni milioni 121.7 kwenye biashara ya wachezaji katika msimu wa 2022-23 na ikiwa ni jumla ya uhamisho uliofanywa baada ya Juni 30, 2023, ambao ulijumuisha kuwasili kwa Jeremy Doku, Mateo Kovacic, Josko Gvardiol na Matheus Nunes, pamoja na kuondoka kwa Cole Palmer, Riyad Mahrez, Aymeric Laporte na James Trafford.



# Neville ana wasiwasi Arsenal kutwaa ubingwa



**LONDON, England**

GWIJI wa soka Gary Neville anaamini kwamba, Arsenal wanaweza kushinda Ligi Kuu ya England msimu huu, lakini bado ana wasiwasi na ubora wa safu ya ushambuliaji waliyo nayo.

Arsenal wameanza vyema msimu huu licha ya kushindwa kufikia kiwango chao cha msimu uliopita ambao walipambana hadi mwisho, wakakaribia kuwa mabingwa, wakaishia nafasi ya pili.

Hivi sasa Arsenal chini ya Kocha Mikel Arteta, ipo nafasi ya tatu kwenye msimamo wa nyuma ya vinara Manchester City waliokusanya pointi 28, wakifuatiwa na Liverpool (27) ambao wana pointi sawa na Arsenal baada ya zote kucheza mechi 12.

"Nafikiri Arsenal wanaweza kushinda ligi msimu huu. Licha ya kuanza polepole, lakini watakuja kukaa sawa mbele na kufanya vizuri kama tulivyoona msimu uliopita.

"Ukweli ni kwamba wameanza polepole kidogo, sidhani kama ni jambo baya. Wasiwasi wangu kwa Arsenal ni mshambuliaji wa kati, nawapenda (Gabriel) Jesus na (Eddie) Nketiah, lakini kwangu mimi hao ni namba mbili na tatu, wanahitaji mshambuliaji namba moja," alisema Neville.

## Mourinho aipa nafasi Inter Milan

**ROME, Italia**

KOCHA Mkuu wa AS Roma, Jose Mourinho anaamini Inter Milan ni timu ya kiwango cha juu sana msimu huu 2023-24, huku Juventus ikiimarika zaidi chini ya Kocha Massimiliano Allegri.

Kocha huyo wa kimataifa wa Ureno alizungumza katika mkutano na waandishi wa habari kama ilivyoripotiwa na FCInterNews.

Lakini akasema bado ni mapema kusema mbio za ubingwa wa Serie A zitakuwa kati ya Inter Milan na Juventus.

Lakini mechi za mwishoni mwa wiki iliyopita AC Milan, Napoli, Atalanta, Lazio na AS Roma zote zilipoteza pointi muhimu, wakati Inter Milan na Juventus zikiibuka na ushindi.

Hii ina maana timu hizo mbili zilizo kileleni zina uongozi kwa pointi nyingi tofauti na timu nyingine msimu huu.

Wakati huo huo, uwiano wa pointi kati ya Inter na Juventus ni ndogo kwenye msimamo. Inter (pointi 29) imezidiwa pointi mbili dhidi ya wapinzani wao Juventus (pointi 31).

Lakini ukweli timu hizo mbili zitamenyana baada ya mapumziko ya kupisha mechi za kimataifa na utakuwa mchezo wa upinzani mkali kutokana na ubora wao msimu huu 2023/24.

"Juventus ambao ni timu nzuri na kocha mzuri pia, lakini kuna timu kama Napoli ambayo ilifungwa dhidi ya Empoli, au Milan iliyochezea kichapo cha mabao 3-2 dhidi ya Lecce," alitania Mourinho.

"Yaani namaanisha, samahani zilitoka sare ya mabao 2-2."

Kocha wa Inter, Inzaghi anasaka ubingwa wa Serie A kwa mara ya kwanza lakini aliwahi kushinda taji la Coppa Italia na alitinga fainali ya Ligi Mabingwa Ulaya msimu uliyopita na kupoteza dhidi ya Manchester City.

HABARI MICHEZO

# SIMBA VINARA KUFUNGA KIPINDI CHA KWANZA

**Na Adam Fungamwango**

MPAKA kufikia raundi ya tisa ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba inaongoza kwa kufunga mabao mengi kipindi cha kwanza cha mchezo.

Simba imefunga mabao 12 kipindi cha kwanza na hakuna timu yoyote iliyofunga idadi hiyo ya mabao ndani ya dakika 45 za mwanzo.

Kwa mujibu wa dawati letu la takwimu, Simba imefunga mabao sita tu kipindi cha pili na kutimiza idadi ya mabao 18 ambayo imepachika mpaka sasa.

Timu hiyo inashika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi ikiwa sawa na Azam FC, ambazo zote zina pointi 19, Simba ikizidiwa bao moja kwani imefunga mabao 18, wakati Wanalambalamba wana mabao 19.

Mabingwa Watetezi na vinara wa Ligi Kuu Yanga na Azam FC wanafuatia kwa kupachika mabao mengi kipindi cha kwanza kila timu ikifunga mabao tisa ndani ya dakika 45 za kwanza.

Yanga inayoongoza kwenye msimamo wa Ligi mpaka sasa ikiwa na pointi 24, imefunga mabao tisa kati ya 26 iliyonayo mpaka sasa hivyo mabao 17 yaliyobaki yamefungwa kipindi cha pili, huku Azam yenye mabao 19 ya kufunga, imepachika mabao 10 kipindi cha pili.

KMC inafuatia nafasi ya tatu kwa kuwa na mabao saba ya kufunga kipindi cha kwanza, huku ikiwa imefunga mabao mawili tu kipindi cha pili, na kuhitimisha mabao yake tisa ya kufunga mpaka kufikia raundi ya tisa ambapo ligi imesimama kupisha mechi za kimataifa.

Timu za Singida Fountain Gate na Mtibwa Sugar ziko nafasi ya nne, kwani zimefunga mabao sita kila moja kipindi cha kwanza.

Singida imefunga mabao 11 mpaka sasa, hivyo mabao matano imeyafunga kipindi cha pili, huku Mtibwa yenye mabao 10, imepata mabao yake manne kipindi cha pili.




Mshindi wa 'Jackpot Bonus' kutoka SportPesa, Maiko Mathew, akishikilia mfano wa hundi baada ya kubashiri kwa usahihi baadhi ya mechi za Jackpot. **PICHA: SPORTPESA**

# Dodoma Jiji kambini kuikabili Singida FG

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Dodoma Jiji kimeingia kambini kuanza rasmi mazoezi kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara raundi ya 10 dhidi ya Singida Fountain Gate itakayochezwa Novemva 24 kwenye Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Kassin Liogope amesema baada ya kushinda mechi mbili mfululizo za ugenini kwa bao 1-0 dhidi ya JKT Tanzania na mabao 2-1 dhidi ya KMC zote zikichezwa jijini Dar es Salaam, waliwapa mapumziko ya muda mfupi wachezaji wao na sasa wamerejea kambini na kuanza mazoezi jijini Dodoma kwa ajili ya kuwavaa Singida.

"Nadhani pia tutacheza mechi kama mbili za kirafiki kwa sababu kutoka leo hii hapa hadi Novemba 24 ni parefu kidogo kwa hiyo tunajitahidi kuwarudisha wachezaji kwenye hali nzuri na wawe na utimamu wa mwili," alisema Liogope.

Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Fortunatus John, ameeleza kufurahishwa na mwenendo wa timu hiyo, akisema kutokana na hali hiyo viongozi wamekaa vikao ili kuhakikisha wanapata ushindi pia katika mechi dhidi ya Singida, ikichukuliwa kuwa wanacheza nyumbani.

"Tunaichukulia kwa umuhimu mechi hiyo kwa sababu tunataka kuhakikisha tunaendelea kuishikilia nafasi ya nne, Singida ni moja kati ya timu ambazo zinacheza pale juu nafasi ya tatu na nne, kwa hiyo ukiifunga ni kwamba unainyima fursa hiyo na sisi tunakuwa salama," John.

Naye mshambuliaji wa timu hiyo, Emmanuel Martin, akizungumzia mchezo huo, alisema kuwa itakuwa mechi ngumu kwa sababu Singida ina kikosi kizuri.

Dodoma Jiji ina pointi 15 ikiwa kwenye nafasi ya nne, imecheza mechi tisa, imeshinda mechi nne, imetoka sare mechi tatu na kupoteza mechi mbili.

## Viongozi Simba wawaweka kitimoto

INATOKA UK. 24

"Wachezaji wanatakiwa kupambana katika michezo yote mitatu ya nyumbani tukianza na Asec Mimosas, tusiwachukulie poa tuliwahi kuwafunga hapa lakini nina imani hawatakuja kiwepesi, tunatakiwa kupambana kutafuta ushindi kabla ya kwenda Botswana katika mchezo wetu wa pili ," alisema Ahmed.

Baada ya mchezo huo wa Novemba 25, Simba itasafiri kwenda Botswana kuumana na Jwaneng Galax ukiwa mchezo wake wa pili na wa kwanza ugenini katika kundi lao.

"Ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kwenda hatua inayofuata ni lazima tupate ushindi kwenye mechi zetu za nyumbani...hii itatupa wepesi wa kusonga mbele," alisema Ahmed.

Kuhusu majeruhi, Ahmed, alisema mpaka sasa kikosi chao hakina majeruhi mwingine zaidi ya Aubin Kramo ambaye anaendelea kuuguza goti kutokana na upasuaji alioufanya hivi karibuni.

"Kibu Denis tayari amerejea kwenye hali yake na yupo kwenye kikosi cha timu ya taifa, Sadio Kanoute pia amerejea kikosi na tayari yuko kambini na wenzake akiendelea na mazoezi, kwa hiyo tunashukuru mpaka sasa hali ipo hivyo," alisema Ahemd.

Katika hatua nyingine, Ahmed amesema kikosi cha wapinzani wao Asec Mimosas kinatarajia kutua nchini Novemba 23, mwaka huu saa 9:40 Alfajiri wakiwa na msafara wa watu 31.

Pia aliwataja waamuzi watakaochezesha mchezo huo kuwa ni mwamuzi wa kati Mohamed Maarouf Eid Mansour akisaidiwa na Samir Gamal, Yousset Wahidi na mwamuzi wa akiba ni Mohmoud Nagy wote kutoka Misri.

Kuhusu viingilio, Ahmed alivitaja kuwa Shilingi 5,000 eneo la mzunguko, VIP C ni Sh. 10,000, VIP B Sh. 20,000, VIP A Sh. 30,000 na Sh. 150,000 kwa eneo la Platinum na bei hizo ni mahususi kwa ajili ya wanasimba wote kuweza kujitokeza kwa wingi uwanjani siku ya mchezo.

"Hii mechi tunawahitaji mashabiki wa Simba, kwa sababu ndio wageni wetu rasmi, kwa sababu ya kuwapa nafasi tunataka kuthamini mchango wao baada ya kupata tuzo ya mashabiki bora hivi karibuni katika mashindano ya African Football League.

"Lakini tunawahitaji sana mashabiki ili kuongeza hamasa kwa wachezaji wetu na kuwa kitu kimoja, tunatakiwa kusahau ya nyuma na sasa tushikamane kwa ajili ya michezo inayofuata hasa michuano hii ya kimataifa," alisema Ahmed.

# Michezo

Ijumaa Novemba 17, 2023

Nipashe




**Man United haitakubali ofa ndogo kwa Sancho** UKURASA 21



Baadhi ya wachezaji wa Timu ya Taifa 'Taifa Stars', kutoka kulia Novatus Dismas, Simon Msuva na Abdi Banda wakiwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere muda mchache kabla ya kuanza safari kuelekea Morocco kwa ajili ya mchezo wao wa kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Niger. **PICHA: BINZUBEIRY**

# VIONGOZI SIMBA WAWAWEKA KITIMOTO WACHEZAJI KAMBINI

## ●●●Wataka kusahau ya nyuma na kujituma zaidi kuipigania klabu katika...

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha wanaanza vizuri na kuvuka hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, uongozi wa klabu ya Simba umewaweka kitimoto wachezaji wake na wamewataka kusahau yaliyotokea nyuma na kujituma kwenye mchezo wao dhidi ya Asec Mimosas watakaocheza nao Novemba 25.

Simba itawakaribisha wa Ivory Coast kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa ukiwa mchezo wa kwanza hatua ya makundi ya michuano hiyo mikubwa kwa ngazi ya vilabu Afrika.

Simba iko kambini chini ya Kaimu Kocha Mkuu, Daniel Cadena akisaidiwa na Seleman Matola kujiandaa na mchezo huo utakaochezwa saa 10: 00 jioni.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema uongozi wa klabu hiyo umekutana na wachezaji na kuwataka kusahau matokeo yaliyopita na sasa akili na nguvu zao kuelekeza katika mchezo huo.

Alisema wachezaji wanatakiwa kufikiria zaidi mchezo huo na kuhakikisha wanakuwa makini katika maandalizi yao na kuwataka wanajitoe na kupambana kwa dakika zote siku hiyo ya Novemba 25.

"Wanatakiwa kutambua kwa sasa wanasimba hawana raha baada ya mechi mbili zilizopita sasa kufuta majonzi yao wanalazimika kupambana katika mchezo huo ambao wageni rasmi ni mashabiki wa Simba.

"Wanatakiwa kusahau yaliyopita na kuingia uwanjani kifua mbele na kuendeleza mazuri, tunaimani kubwa na wachezaji hao kufanya vizuri katika mchezo huo," alisema Ahmed.

Alisisitiza kuwa kikosi kimeingia kambini kwa ajili ya kujiandaa na mchezo huo, lakini michezo mingine iliyopo mbele yao ili kufikia malengo ya kuhakikisha wanakusanya alama tisa za kimataifa katika michezo mitatu watakayocheza nyumbani.

INAENDELEA UK. 23

# Yanga SC kuibomoa tena AS Vita

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI dirisha dogo la usajili likikaribia, klabu ya Yanga inadaiwa kupiga tena hodi Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwenye klabu ya AS Vita ikihitaji huduma ya winga wake Elie Mpanzu kwa ajili ya kuimarisha kikosi chao.

Yanga ambayo kwa kiasi kikubwa imekuwa ikinufaika na wachezaji wengi wanaotoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, hasa kwenye klabu ya AS Vita, inamhitaji Mpanzu kwa udi na uvumba, na kutokana na mahusiano mazuri kati ya klabu hizo mbili, kuna uwezekano mkubwa wa winga huyo mwenye kasi na ufundi kuvaa jezi ya kijani na njano.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema wachezaji Jesus Moloko na Mahlatse Makudubela 'Skudu' ambao hawana namba za kudumu kwenye kikosi cha kwanza kuna uwezekano wakaonyeshwa mlango wa kutokea ili kuruhusu mabadiliko ya wachezaji ambao wataleta ushindani wa namba kikosini.

Mchezaji mwingine ambaye tayari ameshaanza kutajwa kuwa atakuwa kwenye kikosi hicho ni Ranga Chivaviro kutoka Kaizer Chiefs, ambaye wengi wanamuhusisha kutokana na ziara ya Rais wa Yanga, Injinia Hersi S aid, nchini Afrika Kusini hivi karibuni.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe alisema tayari wameshawasiliana na wachezaji wote ambao wanataka kuwasajili na wanaendelea na mazungumzo kabla ya kuwatangaza.

"Kocha Miguel Gamondi, ameshawasilisha ripoti kwa uongozi juu ya maeneo gani yanatakiwa kufanyiwa marekebisho au kuongezewa nguvu, na pia ni aina gani ya wachezaji anaowataka kuja kuongeza nguvu kwenye kikosi chetu, uongozi sasa unafanyia kazi ripoti yake," alisema Kamwe.

Alisema wanafanya mambo yao kwa umakini mkubwa na wanataka dirisha dogo la usajili Januari likifika wawatangaze tu wachezaji watakaokuwa wamewasajili.

Wachezaji ambao Yanga ilishawachukua kutoka AS Vita kwa misimu ya hivi karibuni, ni Moloko, Yannick Bangala, Djuma Shaaban, Fiston Mayele, Tuisila Kisinda na Mukoko Tonombe ambapo hata hivyo ni Moloko tu ndiye aliyesalia kwenye kikosi hicho kwa sasa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >